


# UTUONYESHE BABA

 Asante, Ndugu Rich, ndugu, Bwana awabariki.

<sup>2</sup> Habari za jioni, marafiki. Ninayahesabu haya kuwa ni majaliwa makuu kuwa hapa alasiri ya leo katika utumishi wa Bwana Mungu. Na siku hizi tatu zimemaanisha mengi kwangu kuja huku kukutana na marafiki wa zamani na kupata wapya. Hivyo ndivyo maisha yanavyosonga mbele kwetu, ni kukutana tu na wapya na—na kufurahia urafiki wa marafiki wa zamani.

<sup>3</sup> Halafu basi, chini kupitia Grande Prairie na pia hapa juu, nimepata uchaji halisi miongoni mwa watu na matarajio ya uamsho. Huo ndio mnaohitaji, ni uamsho halisi wa kiroho, kumwagwa kwa Roho Mtakatifu juu ya watu.

<sup>4</sup> Ndipo sina budi kukutana na baadhi ya marafiki zangu wa kale, Chris Berg, yuko hapa mahali fulani, na, ama kwa kawaida huwa, nami nilikuwa nikitarajia kukutana na Milo, naam, Ndugu Durney, ninafurahi kukuona umeketi humu ndani, vizuri sana.

Bw. Durney alikuwa kiongozi wangu mara ya mwisho, tulipoenda, kuwinda. Marafiki zangu hapa wanakumbuka mara nyingi tukizungumzia hilo.

<sup>5</sup> Nasikia ulizingirwa kidogo na maradhi tangu wakati huo. Vema, Bwana niliyekuwa nikinena habari zake pale, angali ni Mungu yeye yule, yule Mponyaji mkuu. Della hajambo? Anaendelea vizuri? Hilo ni sawa.

<sup>6</sup> Bw. Durney alikuwa kweli ni kipande kidogo cha chuma, nawaambia. Alipokuwa na yapata umri wa miaka sabini, nadhani, nilipokuwa hapa juu, naye alikuwa kweli... Nilishangaa kuona nguvu halisi ndani ya—ndani ya mtu huyo kwenye umri huo, yeye, popote mimi na Chris tungeweza kwenda, alikuwa pale pale mbele yetu. Nami nimeninii. . .

<sup>7</sup> Mtu hawezi kuishi huko nje mahali kama hapo bila kumjua Mungu. Kwa hiyo nisingeweza kusimama, kuangalia juu milimani bila kuuona uso wa Mungu mahali fulani. Na mara nyingi nimemwombea rafiki yangu Chris, Bw. Durney, na hao wengine.

<sup>8</sup> Siku moja, maisha yatakapokwisha kabisa, kwenye vijia vya wanyama pori Huko juu katika msitu usio na mwisho, natumaini kukutana nanyi ndugu Huko juu, kufanya upya urafiki wetu. Mtanikuta kwenye baadhi ya vijia vya wanyama kule juu, nitakuwa nikiangalia kote, nitakutana nanyi nyote, marafiki zangu wawindaji na marafiki wategaji, Huko juu siku moja, mpaka wakati huo, tunataka kuwa kazini kwa ajili ya Bwana wetu.

<sup>9</sup> Nilikuwa njiani nikienda zangu, nilikuwa na likizo fupi iliyokuwa ikija, ambayo imekuwa ni miezi sita hudumani, nayo ni, hakika imenichosha, nami niliwazia ningechukua likizo kidogo na kuja kaskazini, huku, nione kama ningeweza kumshika mmoja wa hao wa kijivujivu ninyi ndugu mliokuwa mkiwazungumzia, na labda nimwone dubu barabarani.

<sup>10</sup> Kwa hiyo nikapanda juu, nao wakafanya maandalizi pamoja na mchungaji wenu. Basi Bwana akipenda, alasiri ya leo au mapema asubuhi, mojawapo, tunaondoka kwenda kwa siku chache za mapumziko huko nyikani, tujaribu kurudi tena katika shamba la Bwana.

<sup>11</sup> Nilifikiri lisingekuwa jambo zuri, ingawa nilikuwa mchovu na nimedhoofika kutokana na miezi sita moja kwa moja hudumani, na kazi yangu ni ya kimataifa, kama mjuavyo, ulimwenguni kote, nami nilifikiri ingekuwa sawa kama nikija na kuwatembelea marafiki zangu hapa Dawson Creek na Grande Prairie. Nami ninataka kumshukuru Bwana kwa ajili ya ushirika mkuu ambao tumekuwa nao pamoja pamoja na wachungaji na watu wenye imani moja ya thamani, katika nia moja, na wote wakimpenda Bwana, na wengi wenu ninyi watu.

<sup>12</sup> Billy alikuwa akiniambia nilipoingia, kwamba walimpa sadaka ya upendo alasiri ya leo. Ninaamini hiyo ilikuwa ni kweli. Hakika sikutaka mfanye hivyo, ndugu yangu, dada, mimi kamwe. . . Nimekuja tu kuwatembelea, nami ninathamini jambo hilo hata hivyo.

<sup>13</sup> Basi wakati mmoja, nilikuwa nikiwazia hivi majuzi, walinipa moja, kama baadhi yenu watu wa Grande Prairie mko hapa, hata sikujua lilitendeka mpaka Bw. Sothmann aliponiambia nilipokuwa njiani kuelekea nyumbani, na hata sikuwa na nafasi ya ku—kuwashukuru watu hao wa thamani.

<sup>14</sup> Vema, nijuavyo mimi, itaenda kwa Ufalme wa Mungu, vizuri nijuavyo mimi. Asanteni sana. Nami ninaamini imeandikwa katika Biblia, Yesu alisema, “Kadiri mlivyomtendea aliye mdogo kuliko wote wa hawa watoto Wangu, mmenitendea Mimi.” Mimi ndiye huyo, mdogo kuliko wote.

<sup>15</sup> Nina umri wa miaka hamsini na miwili, nimekuwa nikihubiri miaka thelathini, kamwe sikuchukua sadaka maishani mwangu, kamwe sikuchukua hata senti moja maishani mwangu, kuchukua sadaka. Sikuzote nilifanya kazi, nikapata riziki yangu, na ninapokuja huku, mbona, mimi kamwe. . . ninaingia tu kwenye miji, nao wanalipa gharama za mkutano, ninamaanisha yale majumba makubwa ya mikutano, ambako inakubidi kupata dola elfu moja, mbili, kwa usiku mmoja, mbona, wanalishughulikia tu, wala hainibidi kuwa nazo.

<sup>16</sup> Na daima anaponipa chochote, mbona, daima kuna mahali pa kukiweka, kwa hiyo mnajua ninachomaanisha

nacho. Ni ninii . . . Ninapenda kuishi kwa imani. Hivyo ndivyo tunavyopaswa kufanya, kuishi kwa imani.

<sup>17</sup> Ninaona lesa mbili zimewekwa hapa jukwaani, ama, mimbarani, zipate kuombewa. Sasa, hilo si ushirikina, hilo ni Maandiko, hilo ni Biblia. Wengi wenu, labda, mngataka kitambaa cha maombi; hiyo ndiyo moja ya huduma kuu sana nilizo nazo sasa.

<sup>18</sup> Hapa siku moja, ningeninii . . . nilishangaa, ningeninii . . . Mama mmoja huko Ujerumani . . . Ninatuma maelfu ya hivyo kote ulimwenguni. Basi mama mmoja huko Ujerumani alikuwa na yabisi kavu kwa yapata miaka ishirini ama ishirini na mitano, na—nami nikakosa kumshika huko Ujerumani, tulikuwa na wengi sana, maelfu tu mara maelfu walimiminika kutoka kila mahali, huko Czechoslovakia na kila mahali. Kwa hiyo wao . . . Ughaibuni si kama ilivyo hapa, huko ile—ile miji ni . . . hiyo nchi ni ndogo na watu wengi, na mkutano kama huo huwavutia tu kila mahali.

<sup>19</sup> Na kwa hiyo kulikuwa na maskini mwanamke Mjerumani, alipata maagizo kwenye kile kitambaa kidogo cha maombi, naye . . . Inasema hapo kuwaita marafiki zako au mchungaji wako, kama unaweza, la siyo, mmoja wa majirani, uungame makosa yako yote na umwombe Mungu akuponye, na kukiweka juu yako kisha uamini.

<sup>20</sup> Basi maskini mwanamke huyo Mjerumani, ilikuwa ni ajabu, alikiweka ninii—ninii . . . alikiweka kwenye vazi lake la ndani, kama ilivyoagizwa, akawaita majirani waingie na kuomba. Alikiri makosa yake yote, na alipokiweka pale, akaweka mkono wake juu ya moyo wake, akasema, “Sasa, ewe maskini mzee ibilisi, ondoka kwangu.” Naye moja kwa moja akasimama, akaenda akitembea sakafuni, baada ya kuwa kwenye kiti hicho cha magurudumu kwa miaka *ishirini na kitu*. Ni rahisi tu hivyo.

<sup>21</sup> Mnajua, kuna mara nyingi ambapo sisi hujaribu kufikia kitu fulani, kwa ajili ya namna fulani ya imani. Wala haikubidi kuwa na namna fulani ya imani kuu ku—kuponywa, kitu pekee unachopaswa kuwa nacho ni kuchukua tu imani uliyo nayo.

<sup>22</sup> Mwajua, katika Biblia damu ilipakwa milangoni kwa hisopo; ndugu zetu makasisi wanajua hilo. Hisopo ni magugu ya kawaida tu, na jambo ni kwamba, watu siku hizi wanajaribu kutafuta okidi ya kupaka Damu, na hata haipakwi kwa okidi, inapakwa kwa hisopo, imani ya kawaida tu, ya kila siku.

<sup>23</sup> Kama tu: haikubidi kuwa na imani yoyote kuu sana, ulikujaje hapa? Unajuaje utaondoka? Unawezaje kuendesha gari lako? Unajuaje unaweza kusogeza mkono wako? Vema, unafanya tu bila kuliwazia, kwa sababu unaamini unaweza kufanya hivyo.

<sup>24</sup> Sasa, hivyo ndivyo unavyoamini kwa ajili ya uponyaji wako, imetatuliwa tu na ni hayo tu. Haihitaji elimu fulani ya juu, kitu *fulani* cha ajabu sana, inahitaji tu imani ya kawaida

katika Mungu. Liamini tu jinsi ungelifanya kama mama yako angalisema angekupa kitu, amini tu namna hiyo.

<sup>25</sup> Walichukua damu . . . Hisopo, kwa kawaida wanaiona ikikua katika nyufa za kuta huko Misri na Palestina, walikuwa na kuta za matofali, na—nayo hisopo ingekulia kule juu, ni jani dogo lenye pembe tatu, nao wanaling'oa tu namna *hiyo*, wakaichovya kwenye damu, na kuipaka mlangoni.

<sup>26</sup> Vema, Damu, bila shaka, ikipakwa, tunaipaka kwa imani. Nayo imani ni ya kawaida, kama tu hisopo, magugu tu ya kawaida, amini tu na yote yamekwisha.

<sup>27</sup> Sasa, kama yeyote wenu angetamani kupata kitambaa kidogo cha maombi na hunacho hapa juu, kama utaniandikia tu wakati wowote, nitafurahi kukutumia. Andika tu: William Branham, Jeffersonville, Indiana, nayo itanijia.

<sup>28</sup> Na kama unataka moja ya kuweka tu katika Biblia yako kwenye Matendo 19, iwapo jambo fulani litatukia, mbona, tuma tu. Hakuna malipo kwa chochote, ninii tu, hatulipishi chochote, kila kitu ni bure. Kwa hiyo agizia tu na ukipate, tutafurahia kukutumia, tutafurahia sana. Na ni kitambaa kidogo ambacho nimekiombea na kumwomba Mungu akuponye na akusaidie.

<sup>29</sup> Loo, ningeweza kutumia alasiri nzima nikisimulia tu mambo makuu ambayo amefanya kupitia hicho, mambo makuu, lakini tunajua watu hawana budi kutumia jengo lao hapa usiku wa leo. Nasi hatutaki kuwaweka muda mrefu sana, na kwa namna fulani jengo hili limejaa sana, nanyi mmesongamana sana humu.

<sup>30</sup> Na kwa hiyo sasa, tunataka pia kuwashukuru ndugu zetu wahudumu, kwa moyo wetu wote, kwenu ninyi walei wote, na kwa ushirikiano wenu mzuri. Nami ninataka kuwashukuru nanii wa m—mjini, polisi na kadhalika.

<sup>31</sup> Itanibidi kusema hili juu ya rafiki yangu wa kusini hapa, Bw. Evans, ninapaswa kumwacha aje hapa na kuzungumza kidogo, mpate kusikia ambapo . . . jinsi wakusini wanavyozungumza kweli. Mnafikiri kwamba ninayatamka vibaya! Ninyi . . .

Alikuwa kwenye kituo cha petroli, akasema, “Waweza kuniambia palipo na *moteli*?”

Huyo Mwingereza akamwangalia kwa mshangao sana, akasema, “Naam, nina *matairi makuukuu* hapa.” Matairi makuukuu.

Akashuka na kusema, “Ninataka *aiskrimu* kidogo.”

Mtu huyo akasema, “Hakika.” Akanyosha mkono akachukua kibweta cha *aspirini* na kumpa. Kwa hiyo tunashukuru sana.

<sup>32</sup> Alisema hivi majuzi . . . Nilikuwa nimesimama kwenye duka la mwanaspoti hapa, muungwana mzuri sana nikizungumza naye, nasi tulikuwa tukiangalia nyara zao. Nilikuwa nikijaribu

kumwambia Ndugu Evans jinsi hao kongoni walivyokuwa wakubwa zaidi kuliko sungura wake huko Georgia.

Kwa hiyo tulikuwa tukiangalia zile nyara kubwa zilizotundikwa pale, na kwa hiyo akasema, “Mtu fulani anapata tiketi.”

Kwa hiyo ilikuwa ni Bw. Evans, kwa hiyo akatoka mbio na kusema, “Ngoja kidogo, Ndugu, mimi . . .”

Akasema, “Usijali, usijali.” Kasema, “Nitakupa tu tiketi, ‘Karibu tena Dawson,’” tiketi ya heshima.

<sup>33</sup> Basi akaja na hotuba yake ya kusini, naye akasema, “Ndugu Branham,” akasema, “Laiti ningaliweza kupeleka moja ya hizo huko Georgia kwa ajili ya mbegu.” Hawana urafiki sana hivyo unapovuka mpaka hapa chini.

<sup>34</sup> Kwa hiyo mna nchi nzuri sana hapa, watu wazuri sana. Mna moja ya nchi zilizo nzuri sana, na Bwana Yesu akikawia, katika miaka hamsini kuanzia sasa taifa hili litauongoza ulimwengu. Mna rasilimali, vilima vye—vyenu vimejaa dhahabu na fedha, mna chuma, madini, potashi, kalisi, rasilimali ya kila namna, mbaao, lakini hamna watu wengi.

<sup>35</sup> Jiji la New York lina watu mia mbili na tisini na sita elfu zaidi, katika jimbo la New York, kuliko ilivyo katika Milki yote ya Canada, mnaona, Milki nzima ya Canada, watu mia mbili tisini na sita elfu zaidi. Mnaona, mna nafasi kubwa sana.

<sup>36</sup> Nayo Canada ni moja na theluthi moja ninii . . . , ama, theluthi mbili kubwa kuliko—kuliko Marekani. Mna rasilimali, bali kamwe hamna watu, kwa hiyo mshukuruni Bwana kwa jambo hilo.

<sup>37</sup> Mnaona, mngali . . . Kama ninauza ngano na kukubadilishia na mchele, lakini nitakapoishiwa na ngano, tutafanya nini? Ta- . . . Marekani yetu imeishiwa na rasilimali; mnazo, kwa hiyo Mungu awabariki nazo.

<sup>38</sup> Mna serikali nzuri, imara, na—nasi tunaninii . . . benki zenu zote zinamilikiwa na serikali, na kwa hiyo hakuna mgongano wa Wall Street hapa. Nao watoto wenu wote wachanga wana nafasi kubwa, mna mengi ya kuwapa, kuliko tungaliweza kufanya mahali pengine popote ulimwenguni nijuavyo mimi.

<sup>39</sup> Rafiki zangu, siko hapa kuwaambia hilo, mnajua hilo, lakini niko hapa kuwaambia kitu mnachoweza kuwapa watoto wenu mahali popote, hicho ni Bwana Yesu Kristo, Yeye ndiye Kitu muhimu, kwa sababu moja ya siku hizi, kadiri maskini taifa hili lilivyo mashuhuri, litaanguka hakika tu kama chochote kile, halina budi kufanya hivyo, kufanya njia kwa ajili ya Umilele. Lakini wapeni watoto wenu Kristo, Yeye ndiye Tumaini, Tumaini pekee thabiti tulilo nalo. Mungu awe pamoja nanyi daima sasa.

40 Tunapoinamisha vichwa vyetu kwa muda kidogo tu, kabla ya kulikaribia Neno, ninaamini Neno kwa moyo wangu wote, ninaamini ni Neno la Mungu, kwa hiyo hebu na tumkaribie Mwandishi kabla hatujaomba baraka Zake juu yetu.

41 Mungu Mwenyezi na Mwenye Neema, uliyemfufua kutoka kwa wafu siku ya tatu Bwana Yesu, Mwanao, ambaye, kwa neema Yake, ametusamehe dhambi zetu na kuponya magonjwa yetu bure, twampa Yeye utukufu milele na milele.

42 Tuna furaha kuwa mgeni leo hii miongoni mwa watu hawa wa thamani wa Canada. Hatujisikii kwamba sisi ni wageni, bali sisi ni raia pamoja nao katika uchumi mkuu wa Mungu. Tunakushukuru Wewe kwa ajili ya jambo hili, ya kwamba pamoja tutasimama kama jeshi lililoungana kwa ajili ya Ufalme wa Mungu, tukiwafundisha watu wote na mataifa yote kumwamini Bwana Yesu Kristo, kama vile Wewe ulivyotuagiza kwenda ulimwenguni kote na kuyafanya mataifa yote kuwa wanafunzi.

43 Na kama raia pamoja leo, tunaiunganisha imani yetu, na matumaini yetu, na maombi yetu kwa ajili ya watu walio hapa. Kwa kukusanyika leo, kama kuna wengine hapa, Bwana, ambao hawakujui Wewe kama Mwokozi wao, jalia hii iwe ndiyo siku ambayo watafanya uamuzi huo unaotosheleza kwa yote kwamba “Yesu ni Mwokozi wangu tangu leo na kuendelea.”

44 Kama kuna wale hapa Bwana, walio wagonjwa na wanaoteseka, jalia Uwepo Wako uwe na nguvu sana na ukushinde sana kutokuamini, hata kila mtu hapa ndani ataponywa. Tujalie, Bwana. Jalia kusiwe na mtu mmoja mnyonge miongoni mwetu mwishoni mwa ibada hii.

45 Baba wa Mbinguni, tunapotengana alasiri ya leo kutoka ibadani, kwenda kwenye makazi yetu mbalimbali, sijui, huu huenda ukawa ndio wakati wetu wa mwisho wa kukusanyika upande huu wa Umilele, na kama ndivyo ilivyo, Bwana, kama ndivyo ilivyo, kwamba hatutakusanyika tena pamoja . . .

46 Hapana shaka, kama ningerudi, kama ningeishi na kurudi mwaka mmoja tangu leo hii, wengi watakosekana, basi Baba, tunapaswa kuwa watu wa aina gani? Tunapaswa kuwaendea hawa watu vipi, tukijua labda huu ndio wakati wetu wa mwisho wa kukutana? Kwa unyofu wa ndani kabisa, kwa mioyo yetu yote, huku dhamiri yetu imenyunyiziwa Damu ya Bwana Yesu, jalia tuliendee Neno Lake kwa imani na uchaji.

Basi jalia jambo fulani lifanyiike alasiri ya leo ambalo litawafanya watoto hawa wa Mungu kukua karibu na Wewe.

47 Nami najua hapa leo, Baba, katika jengo hili wako wengi wa hawa, nanii wetu, wale tungeita, watu wa mipakani, wao ni walowezi, ama watoto wa walowezi, wamefanya kazi juu ya udongo. Na nilipokuwa nikipanda njiani hivi majuzi, niliangalia huko nje na kumwona baba, na mama, watoto wadogo miguu

mitupu, waking'oa visiki vya kale kutoka kwenye vinamasi, wakivilundika pamoja, wakijaribu kupanda mbegu ardhini ili wapate chakula, mwaka ujao, moyo wangu ukawaka moto.

<sup>48</sup> Nikawazia, “Ee Mungu, wape Makao ya Milele, ambako hakutakuwako na visiki vya kung’olewa, ambapo hawatapanda na mwingine ale, bali wataishi milele katika Makao yao ya Milele, watoto wao watakuwa pamoja nao.” Tujalie, Bwana.

<sup>49</sup> Wengi wameketi hapa, ambao wanajua maana ya kuufuatilia ujia wa wanyama pori, huko juu kupitia misituni, kuona kuchomoza kwa jua na kutua kwa jua, wanajua ya kwamba katika nyakati za shida kwamba mshiko fulani wa kisiri, kwamba Mungu aliwasaidia, na katika mahali pagumu; ninawapenda, Baba, wao ni ndugu zangu.

<sup>50</sup> Na kama nilivyowaelezea marafiki zangu wazuri wanaoketi hapa leo, natumaini nitakutana nao kote kwenye ujia mkuu wa wanyama pori Utukufuni. Jalia tukutane na wale wote tunaowapenda na tumefanya ushirika pamoja nao hapa duniani. Na kama kuna yeyote ambaye hayuko tayari kwa ajili ya jambo hilo, na wajitayarishe leo.

<sup>51</sup> Ingia katika Neno, Baba, na upande Mbegu mioyoni mwetu kusudi tupate Uzima wa Milele, kwa kuwa tunaomba, katika Jina la Mwanao mpendwa, Mwokozi wetu, Yesu Kristo. Amina.

<sup>52</sup> Karibu inanibidi tu kuanza kwenye Maandiko, kwa sababu ninyi ni watu wazuri sana. Nami sisemi hilo ili tu niwe mwema, ninalisema kutoka moyoni mwangu. Kama ningesema kwa njia nyingine yoyote, ningekuwa mnafiki, na afadhali nikutane na Mungu kama kafiri kuliko mnafiki.

<sup>53</sup> Sasa, ninataka kuwasomea Maandiko, kwa sababu ninaamini ya kwamba yale ningesema huenda yakashindwa, kwa sababu mimi ni mwanadamu, bali Yale asemayo Yeye hayatashindwa kamwe, “Mbingu na nchi zitapita, bali Neno Langu halitashindwa.” Na njia pekee tunayoweza kumkaribia Mungu tukiwa na hakikisho, ni kuja kwa Neno Lake, kwa kuwa Yeye aliahidi kuliheshimu. Katika Yohana Mtakatifu 14:8:

*Filipo akamwambia, Bwana, utuonyeshe Baba, yatutosha.*

*Yesu akamwambia, Mimi nimekuwapo pamoja nanyi. . . siku hizi zote, . . . hamnijui Mimi, Filipo?*

<sup>54</sup> Ningechukua na kutoa muktadha kutoka hapo: *Utuonyeshe Baba*. Hicho ndicho kilio cha moyo wa mwanadamu, kimekuwako sikuzote. Kwa kuwa tunajua ya kwamba kuna Mungu, kila mwanadamu amejaribu kuangalia ng’ambo ya pazia la wakati waone kama wangeweza kuona walikotoka, kwamba kazi yao ni nini hapa, nao watakuwa wapi baada ya kuondoka hapa.

55 Sasa, tunajua tumetoka mahali fulani, nasi tuko hapa kwa sababu fulani, nasi tunaenda mahali fulani. Wala hakuna, kati ya vitabu vyote ulimwenguni, kuna Kitabu kimoja tu Ambacho kinaweza kukwambia unakotoka, wewe ni nani, na unakoelekea, hicho ni Biblia hii. Kwa hiyo tunamkaribia alasiri ya leo.

56 Hata ndicho kitabu cha kale kuliko vyote katika Biblia, Ayubu. Wakati aliposhikwa na majipu, ilionekana kana kwamba kila kitu kilikuwa kimemwendea kombo, ndipo, marafiki wa—wake Wakristo, ama, wa kidini wakasema, “Ayubu, umetenda maovu.” Watu wengi wanataka kusema, kwa sababu mtu fulani ni mgonjwa kwamba alitenda maovu, hiyo si kweli. Ayubu alikuwa mtu mkamilifu, Mungu alisema hivyo.

57 Lakini wakati mwingine Mungu huacha mateso yawapate watu Wake ili kuwajaribu kwa ajili ya imani yao. Alikuwa akimjaribu mtakatifu sio kumkemea mwenye dhambi. Naye Mungu hufanya hivyo apate kujaribu. Yesu alisema . . . Maandiko yanasema kila mwana amjiaye Mungu hana budi kujaribiwa, kupimwa, kufunzwa kama mtoto, na ndipo wanathibitishwa kuwa watoto wa kweli wa Mungu.

58 Na sasa, katika kisa cha Ayubu, wakati utajiri wake wote ulipoondolewa kwake, na watoto wake wote kutwaliwa, marafiki zake wote walikuwa, walimpa kisogo, wakakesha siku saba, wakimshtaki kwamba ni mtenda dhambi kisiri, hata hivyo Ayubu, si . . . alijua yeye hakuwa mwenye dhambi, kwa sababu alisimama imara juu ya yale Mungu aliyokuwa ameahidi. Mungu alihitaji sadaka ya kuteketezwa, naye Ayubu alikuwa ameitoa kwa ajili yake na kwa watoto wake, naye alijua alikuwa amehesabiwa haki, kwa sababu alikuwa ametoa sadaka ya Mungu iliyostahili.

59 Jinsi tungeweza kujifunza kutokana na hilo siku hizi, wakati tunajua ya kwamba tunakuja Mbele za Mungu kwa imani tukiamini, hakuna kitu kitakachobadilisha hilo. Mungu alisema hivyo, na hilo latosha.

60 Ndipo alipodhikika sana na kuketi kwenye lundo la majivu, akijikuna majipu yake, mwili wake ulikuwa umejaa majipu, ndipo mke wake akasema, “Ayubu, kwa nini usimkufuru Mungu ufe?”

61 Akasema, sasa, kamwe hakumwita mwanamke mpumbavu, alisema, “Wanena kama mmoja.” Akasema, “Wewe wanena kama mwanamke mpumbavu. Bwana alitoa, na Bwana ametwaa; libarikiwe Jina la Bwana.” Asingemkufuru Mungu. Alijua ya kwamba hakuwa na kitu, kasema, “Nilikuja ulimwenguni uchi, nami nitarudi uchi.”

62 Ndipo Roho alipomjilia nabii naye akaanza kumwona Mwenye Haki akija, alikuwa akijaribu kupata mahali ambapo angeweza kwenda na kubisha mlangoni Pake [Ndugu Branham anagongagonga mimbarani—Mh.] na kusema, “Ni—ningetaka



kuzungumza na Wewe kwa dakika moja, nina matatizo fulani ningetaka kuyazungumzia. Kwa nini mimi ni mgonjwa? Kwa nini ninateseka namna hii?’ Laiti ningaliweza kuuona mlango Wake, ambapo ninaweza kubisha mlangoni Pake! Ningetaka kumwelezea.”

<sup>63</sup> Ndipo hatimaye, Mungu akanena naye katika upepo wa kisulisuli, kasema, “Jifunge viuno kama mwanamume.” Ndipo Mungu akashuka katika upepo wa kisulisuli, akasema, “Ayubu, ulikuwa wapi nilipoweka msingi wa ulimwengu? Niambie ambapo ekseki zimefungiwa. Wakati nyota za asubuhi zilipoimba pamoja na wana wa Mungu walipopiga kelele kwa furaha, ulikuwa wapi, Ayubu? Kama una hekima nyingi hivi?”

<sup>64</sup> Ndipo Roho akamjia huyo nabii, naye akaona, akasema, “Loo, laiti ningaliweza kumwona Mtu, Mtu aliye na ufahamu ambaye ningeweza kumwendea, Mtu ninayeweza kuwa na imani naye na kusema, ‘Wewe ni Mwakilishi wa Mungu,’ Mtu ambaye angeweza kuweka mkono Wake juu ya mwe—mwe—mwenye dhambi na juu ya Mungu Mtakatifu na kuziba pengo.” Huyo Ndiye tunayemtafuta, Mtu anayeweza kumwekea mkono mwenye dhambi pamoja na Mungu Mtakatifu na kusimama katika pengo.

<sup>65</sup> Ndipo basi, huku ikiwa ni miaka elfu mbili kabla yule Mwenye Haki kuja, aliona ono, naye akapiga mayowe alipoliona, kwa sababu ngurumo zilinguruma, radi ikamulika, naye nabii huyu akaingia katika Roho, aliona ono. Ndipo akasimama na kusema, “Ninajua Mkombozi wangu yu hai, na katika siku za mwisho Yeye atasimama juu ya nchi. Ingawa mabuu ya ngozi yatauharibu mwili huu, hata hivyo katika mwili wangu nitamwona Mungu, ambaye nitamwona mwenyewe, macho yangu yatamwona wala si mwingine. Kwa kuwa hatukuleta chochote humu ulimwenguni, ni hakika hatutoi chochote. Bwana alitoa, na Bwana ametwaa; libarikiwe Jina la Bwana.”

<sup>66</sup> Alikuwa amepata faraja hiyo, alipata Kitu fulani hicho ambacho—ambacho kingeweza, Mtu fulani ambaye angeweza kusimama katika pengo na angeweza kufanya maombezi kati ya mtu mwenye dhambi na Mungu Mtakatifu.

<sup>67</sup> Nina furaha sana alasiri ya leo, enyi kanisa, kwenu, marafiki zangu ambao nimenena juu ya kazi zenu ngumu, kufanya kazi ngumu, na upendo wenu, na machozi, nina furaha leo kwamba pia tumempata Huyo ambaye anaweza kusimama katika pengo na kufanya maombezi kwa ajili yangu na yenu, ambao hatustahili. Ningetaka kuzungumza juu ya kumwona Yeye na kuwaonyesha tu jinsi ilivyo rahisi.

<sup>68</sup> Mara nyingi tunawapeleka wanafunzi wetu, watoto wetu, shuleni kwa ajili ya elimu ya juu, na pasipo kupuuza hiyo, Mungu akataze, hiyo ni sawa, inachangia, inatimiza sehemu fulani, ila

si sehemu muhimu, mara nyingi tunawapeleka mbali na Mungu kwa elimu.

<sup>69</sup> Kamwe hatutamjua Mungu kwa elimu, huwezi. Tuliona hilo sasa kwa kuwa inahitaji mtu . . . Elimu ndiyo adui mbaya kuliko wote ambaye Injili imewahi kuwa naye. Sasa, chunguzeni tu hilo tena mwone hilo. Mwanadamu anafikiri tu anaweza kumshinda Mungu akili, hawezi kufanya hivyo, akili zake ni mwanadamu tu, Mungu ni Roho, asiye na kikomo. Sasa, tunaona . . .

<sup>70</sup> Sasa nataka kuzungumza juu ya kumwona Mungu. “Utuonyeshe Baba, yatutosha.” Yesu alikuwa amesema mengi sana juu ya Baba Yake, naye Filipo alitamani *sana*, mpaka angeninii . . . aliwaambia tu, “Sasa, msifadhaike mioyoni mwenu kwa sababu ninakaribia kuwaacha, mmemwamini Mungu, niaminini na Mimi,” alizungumza kuhusu Nyumba ya Baba.

Ndipo Filipo akaingilia na kusema, “Utuonyeshe Baba, yatutosha.”

<sup>71</sup> Akasema, “Nimekuwako pamoja nanyi siku hizi zote, Filipo, usinjue? Yeye aliyemwona Baba . . . Yeye aliyeniona Mimi amemwona Baba. Basi mbona wasema, ‘Utuonyeshe Baba?’”

<sup>72</sup> Sasa, ningetaka kuuliza alasiri ya leo: Je, mngependa kumwona Mungu? Hivi kweli mngetaka kumwona Huyu tunayemzungumzia? Angeweza kuonekana?

<sup>73</sup> Tulizungumza juu ya hilo usiku wa kwanza hapa. Lakini nitaonyesha njia nne mbalimbali tunazoweza kumwona Mungu. Sasa, nitazungumza juu ya masomo manne upesi sana: “Mungu Katika Ulimwengu Wake,” “Mungu Katika Neno Lake,” “Mungu Katika Mwanawe,” “Mungu Katika Watu Wake.” Na labda kwa njia hiyo tutaweza kujua Mungu ni nini, mahali alipo. Ameondoka? Je, Yeye alikuwa ni kitu kilichoishi wakati mmoja na sasa kimekufa? La, bwana.

<sup>74</sup> Alisema, “Sitakuacha kamwe, wala sitakupungukia. Tazama, niko pamoja nawe sikuzote, hata ukamilifu wa dahari. Bado kitambo kidogo na ulimwengu hautaniona tena, bali ninyi mtaniona, kwa kuwa nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu hata ukamilifu wa dahari.”

<sup>75</sup> Sasa, nitazungumza kwanza juu ya “Mungu Katika Ulimwengu Wake.” Hebu na tuangalie kote sasa tuone kama tunaweza kumwona Yeye. Na kama ninaweza, kwa Maandiko, kuthibitisha ya kwamba Mungu Mwenyezi yuko mumu humu katika chumba hiki alasiri ya leo, hakika linapaswa kutatua swali la kama ungemwamini au la, lakini kwa Maandiko na kwa ushahidi, nithibitisha ya kwamba Yeye yupo papa hapa sasa.

<sup>76</sup> Mnaangalia juu Yake wakati wote, mkijaribu kumtafuta, mnarukia kitu fulani *huko* nje kabisa, wakati kiko papa *hapa*. Biblia inasema ya kwamba Mungu yuko karibu nasi kuliko

mikono yetu, viungo vyetu vya miili yetu, kwa sababu Yeye ni sehemu yetu, Yeye ni Uhai wetu.

<sup>77</sup> Si muda mrefu uliopita, nikizungumza juu ya Mungu katika ulimwengu Wake, nilikuwa na mzee aliyehudhuria kanisa langu jina lake James Wiseheart. Alikuwa ni mzee mvuvi, nilimwita “Uncle Jim.”

<sup>78</sup> Alikuwa na umri wa karibu miaka themanini, naye alikuwa akivua samaki huko mtoni, angekuja kanisani, alikuwa Mkentaki, nao huo mto una upana wa maili moja hivi na, loo, saa nzuri ambazo mimi na maskini Uncle Jim tumekuwa nazo mtoni pamoja, tukiwakamata hao kambare, tukalala ufukoni usiku kucha pamoja na kuzungumza juu ya Mungu na kushikana mikono na kulia kama watoto wachanga. Yuko Ng’ambo ya pili alasiri ya leo, ninatarajia kumwona siku moja, nitakapovuka.

<sup>79</sup> Neno la mwisho nililomsikia akiniambia, nilipokuwa nikija Canada, hapa miaka michache iliyopita, alisema, “Siku moja, Billy Boy, utarudi, na Uncle Jim atakuwa ameondoka.” Yapata siku mbili baadaye, akaanguka ghafla, akafa kwa mshtuko wa moyo, akaenda Nyumbani kukutana na Mungu.

<sup>80</sup> Kulikuwa na kanisa fulani mjini mwetu ambamo familia moja ndogo ilihudhuria kanisa hili, nalo hilo kanisa lilikuwa tu kama dhehebu lililoamini ya kwamba kuna . . .kwa namna fulani lilifundisha Mungu kuwa Kitu fulani cha kihistoria. Na kwa hiyo kulikuwa na mvulana mdogo katika darasa lake la shule ya Jumapili, alikuwa ameshikwa na shauku, naye akamwambia mama yake, akasema, “Mama, kama Mungu ni mkuu hivi, na . . . mbona siwezi kumwona?”

“Mbona,” mama akasema, “mwanangu, sijui.”

Kasema, “Je, ninaweza kumwona?”

Akasema, “Sijui. Kwa nini usimwulize mwalimu wako wa shule ya Jumapili?”

<sup>81</sup> Na kwa hiyo wao . . .mvulana mdogo, kwenye shule ya Jumapili iliyofuata, kasema, “Mwalimu, ninataka kukuuliza jambo ambalo mama ya—yangu hawezi kujibu.” Kasema, “Je, mtu yeyote anaweza kumwona Mungu?”

“Mbona,” akasema, “sijui.” Akasema, “Mwulize mchungaji.”

<sup>82</sup> Kwa hiyo huyo mvulana mdogo katika . . .kwa shauku yake akamwendea mchungaji na kusema, “Mchungaji, nataka kukuuliza swali ambalo mama yangu wala mwalimu wangu wa shule ya Jumapili asingeweza kunijibu.” Kasema, “Mungu huyu mkuu unayenena habari zake, kwani Yeye si Mungu wa jamii ya wanadamu?”

“Naam, mwanangu. Kwa nini?”

Kasema, “Iwapo Yeye ni Mungu, basi mtu yeyote anaweza kumwona? Ningependa kumwona.”

“Loo,” akasema, “mwanangu, la. Hakuna mtu anayeweza kumwona Mungu. Mungu si wa kuonekana.”

<sup>83</sup> Huyo mvulana mdogo akavunjika moyo. Kwa hiyo alikuwa akienda mtoni pamoja na maskini Ndugu Wiseheart kuvua samaki. Siku moja wakishuka, huku Ndugu Wiseheart akiwa na ndevu zake zenye mvi nchani, alikuwa na umri wa kama miaka sabini na mitano, nao walikuwa wamepata mvuo mzuri huko juu mtoni nao walikuwa wakishuka, dhoruba ikatokea, nayo ikawasukumia ufukoni.

<sup>84</sup> Nao wakaenda ufukoni, nao wakupumzika mpaka dhoruba ilipokwisha. Wakaingia chini ya baadhi ya miti na kurudi chini ya mimapo mikubwa na kadhalika, mpaka dhoruba ilipokuwa imepita. Ndipo baada ya hiyo dhoruba kwisha, waliusukuma mtumbwi na kuanza kuteremka mtoni.

<sup>85</sup> Nayo mawimbi madogo, basi mtu wa makasia ndiye tu anayejua jinsi ilivyo kukabiliana na tatizo hilo la kupiga makasia kama... dhidi ya mawimbi, mshindo mdogo wa mawimbi. Nalo jua lilikuwa likitua magharibi, na nyuma upande wa mashariki walikotoka, maskini huyo mvulana alikuwa ameketi kwenye shetri ya hiyo mashua, na kulikuwa na upinde wa mvua, uliotokea angani, kama vile Mungu alivyotoa ahadi ya kwamba ulimwengu hautaangamizwa tena kwa maji.

<sup>86</sup> Basi maskini mvuvi huyo alipoanza kuvuta makasia haya, aliendelea kuuangalia upinde huo wa mvua, na baada ya kitambo kidogo, wakaona machozi meupe makubwa mno, yakilengalenga, yakitiririka mashavuni mwake, kwenye ndevu zake zilizojaa mvi nchani. Ndipo huyo mvulana mdogo akamtazama yule mzee kwa dakika chache tu, akashikwa na shauku sana, akakimbia hadi katikati ya mashua, akaangukia pajani mwa huyo mzee mvuvi, naye akasema, “Bwana, nitakuuliza jambo ambalo mama yangu, au mwalimu wa shule ya Jumapili, au mchungaji anaweza kujibu.” Akasema, “Je, mtu yeyote anaweza kumwona Mungu?”

<sup>87</sup> Maskini huyo mvuvi, akilemewa na swali la maskini mvulana huyo, alivuta makasia yake kwenye mashua, akamkumbatia huyo mvulana mdogo, na kumshikilia kifuani mwake, huku analia, akasema, “Mungu, aubariki maskini moyo wako, kipenzi. Yote ambayo nimeona kwa miaka hamsini iliyopita yamekuwa ni Mungu.” Alikuwa na Mungu sana ndani yake, hadi angeweza kumwona kila mahali.

<sup>88</sup> Hivyo ndivyo unavyomwona Mungu, ni kumwingiza Mungu ndani yako. Ikiwa una kushuku, na—na kushangaa, na fadhaa, na mashaka, kamwe hutamwona Mungu. Inakubidi kumwacha Mungu aingie ndani yako, ndipo atayafungua macho yako.

<sup>89</sup> Sasa, kwa mfano, niliona wakija hivi majuzi, ambapo mabata wetu wote, kutoka huko chini Indiana, walipanda kuja huku kuwatembelea ninyi Wakanada. Wao ni kiumbe

kinachoshirikiana. Nao huja huku kwa sababu moja, kutengeneza kiota. Watarudi huko chini, Indiana tena, kwa hiyo, huko chini Texas na Georgia; wanashuka kuja kuwa pamoja nasi kwenye majira ya baridi kali, wanakuja huku kwenye. . . majira ya kuchipua kuwatembelea ninyi nyote.

<sup>90</sup> Ndipo wakati wao. . . Ninajua hilo ni neno baya sana, *ninyi nyote*, lakini kumbukeni mimi ni—mimi ni mwasi, kwa hiyo. . . Nao wanapokuja hapa, wanaenda kwenye kinamasi hapa, katika vidimbwi vyenu vidogo na kwenye maziwa yenu, nao wanatengeneza maskini viota vyao, wanaangua vifaranga vyao vya bata na—na ninii yao. . . wanaogelea kote kwenye ziwa hili, mpaka baada ya kitambo kidogo inakuja theluji na—nayo inashuka juu ya kilele cha milima. Mnamo Septemba, wakati upepo huo wa kwanza baridi unaposhuka kwenye nyanda hizi za nyasi hapa. . .

<sup>91</sup> Sasa kumbukeni, maskini hao mabata wadogo hawajawahi kutoka kwenye kidimbwi hicho, walizaliwa mumo humo. Nao ni mabata wakubwa sasa, wamekomaa. Na kuna mmoja miongoni mwao aliyezaliwa kiongozi, Mungu alimfanya kiongozi. Basi mara ya kwanza upepo huo unapovuma, hajawahi kuuhihi huo hapo kabla, lakini anajua kuna kasoro. Anafanya nini? Anakimbia moja kwa moja katikati ya kidimbwi hicho pamoja na maskini hayo makasia, anauchomoza maskini mdomo huo hewani na, “*Honk-honk, honk-honk.*” Ndipo kila bata kwenye hicho kidimbwi atamjia moja kwa moja.

<sup>92</sup> Atafanya nini? Ataruka moja kwa moja kutoka kwenye kidimbwi hicho pamoja na kila bata pale, na aende tu moja kwa moja Louisiana awezavyo kwenda. Anajuaje kwenda? Kwa nini?

<sup>93</sup> Tunasema, “Silika, silika humwongoza.” Vema, kama silika inaweza kumwongoza bata kutoka nchi iliyoganda hadi kwenye usalama, ni zaidi sana vipi Roho Mtakatifu anavyopaswa kuliongoza Kanisa la Mungu aliye hai? Shida yake ni kwamba hatumtambui, tunawasikiliza viongozi wetu, viongozi hao wa kujibunia, badala ya Kiongozi aliyetolewa na Mungu, ambaye ni Roho Mtakatifu. Tunawasikiliza maaskofu na maaskofu wakuu na makadinali na makasisi, wakati tunapaswa kuwa tukimsikiliza Roho Mtakatifu, kwa kuwa Huyu ndiye aliyetolewa kuliongoza Kanisa.

<sup>94</sup> Billy Jr., mahali fulani hapa, mimi na yeye tulikuwa tu tumekuwa India miaka michache iliyopita, nami nikachukua gazeti la Kiingereza, ambayo ni nchi ya lugha mbili, nalo lilisema, “Nadhani matetemeko ya ardhi yamekwisha, kwa sababu ndege wanarudi.” Nikasoma makala hiyo kwa undani. Yapata siku mbili kabla ya tetemeko la ardhi kupiga. . .

<sup>95</sup> Huko India sio matajiri kama mlivyo huku Canada. Inawabidi kuokota mawe kondeni kujenga nyumba zao na—na kujenga ninii, nyua za—zao na kadhalika. Nao maskini ndege

wanaingia mle na kujenga viota vyao kwenye mianya hii, halafu kwenye nyua, kondoo wanaingia, alasiri, ng'ombe, na kusimama kwenye kivuli, ambapo jua, hiyo miali ya moja kwa moja ya jua hilo la kitropiki huwapiga, na kuna joto kali. Kwa hiyo daima wangekuja alasiri na kusimama kwenye vivuli vya hizo kuta, zile kuta kubwa ndefu, nao maskini hao ndege wangejenga viota vyao na kuishi katika maghuba haya madogo huko nyuma miambani.

<sup>96</sup> Lakini siku moja, kwa ghafla maskini hao ndege wote, kwa sababu isiyojulikana, wakaruka kutoka kwenye hizo kuta, nao ng'ombe na kondoo hawakuingia kusimama karibu na hizo kuta, walijua jambo fulani lilikuwa linaenda kutukia. Ilikuwaje? Siku ya pili hawakuingia. Basi mnajua jinsi walivyopata kivuli? Waliegemeana na kufanyiana kivuli.

<sup>97</sup> Nafikiri Kanisa linapaswa kujifunza jambo hilo. Ninyi Wamethodisti, Wabaptisti, Wapentekoste, na Wapresbiteri, hivi hamjui, ndugu, ya kwamba inatupasa tuwe tukiegemeana, kuegemeana kufanyiana kivuli, tukijaribu kusaidiana, sio kujaribu kulaumiana, bali kujaribu kutengeneza kivuli kidogo, kivuli kidogo cha Injili cha kusimamia, kwa kuwa tunaishi katika wakati wa uchovu.

<sup>98</sup> Mara, yapata mapambazuko kesho yake asubuhi, kukatokea tetemeko la ardhi, moja baada ya lingine, mpaka likazibomoa hizo kuta. Kama hao kondoo wangekuwa wamesimama kuzunguka hizo kuta, wangeangamia, ng'ombe pia, maskini hao ndege wangalikuwa nyumbani mwao ka—katika hizo kuta, wangeangamia. Lakini ni kitu gani? Mungu yeye yule aliyewaingiza kondoo, na ng'ombe, na ndege kwenye safina, anathibitisha ya kwamba Yeye angali ni Mungu yeye yule, 1960.

<sup>99</sup> Aliwaonya wanyama Wake kuikimbia ghadhabu ijayo, Yeye anaweza pia kuwaita nani Wake. . . Nami nilichukua mkato wake kutoka kwenye gazeti. Ndipo baada ya mngurumo wa mwisho wa hayo matetemeko ya ardhi, maskini ndege hao wakarudi, nao ng'ombe wakarudi.

<sup>100</sup> Ni kitu gani? Mungu katika ulimwengu Wake, Mungu akinena na maumbile, inaonyesha ya kwamba Yeye ni Mungu yeye yule aliyekuwa katika wakati wa Nuhu, ni Mungu yeye yule leo. Na kama ndege na wanyama wangali wanaweza kuongozwa na silika, ambayo ni kitu walichopewa na Mungu, ni zaidi sana vipi. . . inatupasa kwa Roho Mtakatifu kuikimbia ghadhabu ijayo? Kwa kuwa sote tunajua ya kwamba majina yetu yako kwenye bomu la haidrojeni la Urusi mahali fulani. Kwa nini tusiikimbie hiyo ghadhabu? Tunajua kama tukifa katika dhambi, kuzimu kungekuwa maangamizi yetu.

<sup>101</sup> Naye Mungu, kama alivyoahidi katika siku za mwisho, kutuma ishara zizi hizi na maajabu mnyoona yakifanywa sasa Kanisani, kuwa ndiyo ishara ya kuonya ya siku za mwisho. Nasi

tunaiangalia na tungali tunabaki katika vibanda vya kale vya matope vya ulimwengu, tungali tunakaa katika kutokuamini kwetu. “Mungu katika ulimwengu Wake.”

<sup>102</sup> Ninataka kusema hivi kwa ajili ya wawindaji wenzangu: Kama wengi wenu mjuavyo, mimi ni kiongozi huko Colorado, nilifanya kazi kwenye ranchi huko juu kwa miaka kadhaa. Nami nilikuwa nikikumbuka nyakati ambazo sisi . . . Bonde la Mto Troublesome ni . . . Shirika la Hereford hulisha mifugo kwenye bonde hilo. Kama unaweza kuchangia tani moja ya nyasi kavu, unaweza kuweka ng’ombe mmoja msituni upande *huu* tu wa Bustani ya Estes na msitu wa Arapaho, lakini ranchi yako haina budi kuchangia tani moja ya nyasi kavu, na halafu, bila shaka, unawapiga chapa mifugo wako huko. Sininii . . . Naamini mnafanya hivyo huku Vernon, Ndugu Schultz, mngali mnawapiga mifugo yenu chapa hapa, na hiyo ni kuwazuia wasichanganyikane.

<sup>103</sup> Halafu basi, wana uzio unaosogea ambapo ng’o—ng’ombe hushukia kusudi wasirudi nyuma kwenye mali ya kibinafsi. Mlinzi alikuwa akisimama pale. Basi wakati tungewaleta mifugo huko baada ya mkusanyiko wa majira ya kuchipua na kuwaleta tuwaweke malishoni, tulikuwa tukiwapeleka kule juu. Na mara nyingi nimeketi huku mguu wangu umelazwa nchani mwa tandiko, na kumwangukia huyo mlinzi akiwachunguza wanapopita.

<sup>104</sup> Loo, kuna chapa za kila namna. Tulikuwa, naamini, tulikuwa na . . . moja iliitwa Tri—Tripod, na jirani yangu alikuwa Turkey Track, na—na hiyo nyingine ilikuwa, Grimes, upande ule mwingine, ambaye alikuwa mfugaji mkubwa kuliko wote hilo bonde, alikuwa na m—mkuo, Diamond Bar, na kulikuwako na chapa nyingi mbalimbali.

<sup>105</sup> Lakini mwajua, niliona ya kwamba huyo mlinzi kamwe hakujali sana hizo chapa, lakini kuna kitu kimoja alichochunguza kwa makini, hicho kilikuwa ni kile kibandiko cha damu, kwa sababu hakuna kitu kingaliweza kulishwa kwenye malisho hayo ila Hereford wa ukoo safi, kwa sababu wote walikuwa wamesajiliwa, naye akachunguza hicho kibandiko cha damu.

<sup>106</sup> Mara nyingi nimewazia hivyo ndivyo itakavyokuwa kwenye Siku ya Hukumu. Tunaposimama pale, Yeye hatajali tumevaa chapa gani, bali Yeye ataangalia Damu ya Mwanawe aone kama tumeikubali Hiyo.

<sup>107</sup> Mwaka mmoja huko juu tukiwinda, ningeninii . . . theluji ilikuwa haijaja bado, kwa hiyo ku—kulungu walikuwa huko juu, nami nilikuwa nikitafuta kulungu huko juu. Naye Bw. Jeverez, bosu wa hiyo ranchi, basi alikuwa amerudi katika sehemu nyingine, nami ningemchukua katika siku chache. Lakini tulikuwa tayari tumewaondolea mbali, tunaowaita, “kuruta,”

wawindaji wetu, na kwa hiyo tulikuwa huko juu sana kutafuta nyara.

<sup>108</sup> Nami nilikuwa huko juu, kwa sababu theluji haina budi kuwafukuza hao kulungu, wao ni viumbe mwitu. Nami nilikuwa nikitembea, na wakati huo wa mwaka kutakuwa na the—theluji, halafu mvua, kisha jua lichomoze na kadhalika.

<sup>109</sup> Ndipo kukaja dhoruba ya mvua, nami nikaingia tu nyuma ya miti, karibu na mpaka wa msitu. Basi nilipokuwa nyuma ya mti, nilikuwa tu nimesimama pale nikiwazia, “Ee Bwana Mungu wangu! Ninashangaa sana, jinsi, na katika nyota angani katika huu ulimwengu mkuu, Wewe ni Mungu!” Mvua ikakoma, huko nyuma kabisa magharibi jua likachomoza kupitia mwanya wa huo mlima, lilionekana kama jicho kuu la Mungu likiangalia. Na kwa sababu ya mvua na barafu iliyoning’inia kwenye huo usiokauka, upinde wa mvua ukatokea kote kwenye hayo magenge.

<sup>110</sup> Nami nikaangalia kule juu, nikasema, “Ee Mungu, ni vizuri sana kuwa hapa juu! Wewe huyo hapo katika upinde wa mvua.” Na papo hapo, mbwa mwitu akalia juu ya kilima, na—naye mwenziwe akamjibu huko chini kabisa. Na jinsi ninavyoyapenda maumbile, ulimwengu wa Mungu!

<sup>111</sup> Ningeweza kumsikia Mungu katika mlio wa mbwa mwitu. Kisha nikamsikia maskini kulungu dume, aliyepotea katika dhoruba kutoka kwenye kundi lingine. Hapo, nikisimama pale huku mikono yangu imeinuliwa juu hewani, nikilia kwa sababu ningeweza kumwona Mungu katika machweo ya jua, ningeweza kumwona katika upinde wa mvua, ningeweza kumsikia katika kilio cha mbwa mwitu akimlilia mwenziwe, ningeweza kumsikia katika mlio wa kulungu kwa ajili ya kundi lake. Mungu yuko katika ulimwengu Wake, ndugu, hakika yuko.

<sup>112</sup> “Loo,” nikawaza, “watu wanawezaje kukosa kuangalia hilo?” Nikawaza, “Ni vema kuwa hapa.” Kama vile Petro alivyosema, “Na tujenge vibanda vitatu,” lakini huko chini ya huo mlima. . .Nikawaza, “Bwana, kwa nini inibidi. . .? Nilizaliwa kwa ajili ya huu, nilizaliwa nikaishi mlimani, ninaupenda huu, basi kwa nini kamwe inilazimu kushuka huko chini? Lakini bila shaka, kuna watoto wagonjwa huko chini ya mlima, pamoja na baba na mama wasiomjua Mungu, lazima niondoke mahali hapa na kushuka.”

<sup>113</sup> Nilipokuwa nimesimama pale, vema, kwenu ninyi Wapresbiteri, nadhani nilishikwa na mhemuko, kwenu ninyi Wapentekoste, nilikuwa nikipaza sauti, nilifurahi sana, mpaka nikaanza kutupatupa mikono yangu juu, kisha nikaanza kukimbia kuzunguka na kuzunguka mti huo, huku nikipiga mayowe kwa sauti yangu yote, nikimsifu Mungu. Kwa nini? Nilimwona katika ulimwengu Wake, hakika.



114 Nami nilikuwa tu nikipiga mayowe. Kama mtu angekuja mwituni, wangeninii, wangedhani walikuwa na mwendawazimu mwituni, lakini nilikuwa yapata maili thelathini na tano kutoka kwenye ustaarabu. Nami nilikuwa nikikimbia, sikujali, sikutaka mtu yeyote anisikie, nilikuwa nikimsifu Mungu wangu, ambaye ningeweza kumwona katika ulimwengu Wake, kumsikia katika wanyama Wake, kumwona katika kutua jua Kwake, kumwalia katika upinde Wake wa mvua, nikawaza, “Kila kitu hapa ni Mungu.”

115 Yeye yuko karibu kuliko mkono wako wa kulia, unakosa tu kumwona. Ua linawezaje kukua bila Mungu? Sayansi yote ulimwenguni haiwezi kufanya jani moja la lile kangaga. Wanaweza kufanya kitu kinachofanana nalo, bali hawawezi kulifanya hilo kwa sababu lina uhai ndani yake. Mungu ndiye Uhai pekee uliopo.

116 Ni nani angeweza kuangalia usoni mwa yu–yungiyungi na kusema hakuna Mungu na bado adai ana akili timamu? Asingeweza kuwa na akili timamu. Pamoja na sayansi yetu yote, tusingeweza kufanya yungiyungi. Hebu nifanyie mti, mtu fulani. Huwezi. Nifanyie jani la nyasi. Huwezi. Huyo ni Mungu, Mungu katika maua Yake, Mungu katika jua Lake, Mungu katika ulimwengu Wake, Mungu katika wanyama Wake, Mungu katika maumbile Yake, kitu fulani kulihusu.

117 Ninakumbuka wakati mmoja, mimi na Baba yangu tulikuwa tukilima, nasi tulikuwa tukilima mahindi, nami nilikuwa mvulana mdogo tu na farasi wangu akaanza tu kukoroma *hivyo*, huko Indiana shambani, nami nikasema, “Kuna nini?” Walikuwa wakiangalia juu. Nikasema, “Labda mnyama anakuja.”

118 Loo, namwona maskimi baba yangu, wakati huo alikuwa na yapata, yapata umri wa miaka thelathini, nadhani, labda thelathini na mitano, akasimama, akasema, “Billy, mwanangu, nataka kukwambia jambo fulani.” Akasema, “Farasi hao hawaoni chochote.” Kasema, “Lakini unajua kinachokaribia kutukia?”

Nikasema, “La, Baba.”

Akasema, “Dhoruba inakuja.”

“Vema,” nikasema, “sasa, babangu, sioni wingu lolote hata kidogo, wala sisikii ngurumo, wala kuona radi.”

Akasema, “Si lazima, huwezi kuiona bado, wanaweza kuiona.”

Nikasema, “Sielewi. Unamaanisha macho yake ni bora kuliko yangu?”

119 Akasema, “Si lazima, lakini unaona, Billy, Mwenyezi Mungu ameweka katika maumbile njia ya kujihifadhi na kujidumisha yenyewe.” Kasema, “Farasi huyo anaweza kunusa ama kuhisi

dhoruba hiyo,” kisha kasema, “Mungu huwapa hiyo ili waweze kufika kwenye usalama.”

<sup>120</sup> Nikasimama pale kidogo, baba yangu hakuwa Mkristo wakati huo, kwa hiyo nikawazia, “Hakika, kama Mungu anaweza kumpa farasi hisia ya kufika kwenye usalama wakati shida inakuja, ni zaidi sana jinsi gani anavyoweza kuwapa watoto Wake?” Yeye yuko katika ulimwengu Wake. Mnaona?

Karibu, tukalima raundi mbili zaidi kisha nikasikia ngurumo, wingu lilikuwa juu yetu katika nusu saa nyingine. Wangeweza kuihisi.

<sup>121</sup> Basi nikiendelea kwenye huo mlima, wakati nikisimama pale, nami nilikuwa nikiuzunguka na kuzunguka mti huu, nikifurahi tu kwa moyo wangu wote. Mnajua, mimi, ninapojisikia kubarikiwa, ninajisikia sasa hivi, kwa namna fulani ni—ninashikwa na mhemuko, na—nakisia mnaweza kuuita ulokole, lakini mtu fulani alisema, “Billy, unafanya kana kwamba huna akili timamu.”

<sup>122</sup> Nikasema, “Vema basi, niache tu, kwa sababu ninajisikia vizuri zaidi *hivi* kuliko nilivyojisikia vinginevyo. Kwa hiyo kama sina akili timamu, hebu niweke tu *hii*, kwa sababu ninaifurahia hii zaidi, nikimjua Mungu ndani yake.”

<sup>123</sup> Na kwa hiyo nikauzunguka na kuzunguka ule mti, nami nilikuwa nimesimama huku nimeinua mikono yangu, nikisema, “Mungu, Wewe ni Baba yangu. Loo, ninakupenda, Wewe, uliyeyamba huu mlima, na kunifanya niufurahie, ukawaumba wanyama mwitu. Nami hapa nimesimama nikiogelea katika Uwepo Wako. Kwa nini watu hawawezi kukuona katika ulimwengu Wako mkuu?”

<sup>124</sup> Wanawezaje kuelezea dunia hii kusimama kwenye matundu, ikining’inia hewani namna hii, ikizunguka kikamilifu, na imewekewa wakati vizuri *sana*, hata wanajimu wanaweza kujua ile dakika hasa ambapo kupatwa kwa mwezi kutakuja, kati ya mwezi na jua miaka ishirini, na miaka thelathini kabla ya wakati?

<sup>125</sup> Hakuna kipande cha mtambo wowote uliowahi kubuniwa unaoweza kuisogeza hiyo, hauwezi kuisogeza kikamilifu hivyo. Saa yako haitafanya hivyo, hakuna saa inayoweza kudumisha wakati mkamilifu, si kwa muda wowote wa wakati. Itapoteza pigo moja ama mawili, ama kuongeza pigo moja ama mawili. Ha—hakuna kitu ambacho mwanadamu anaweza kufanya namna hiyo, bali Mungu ni mkamilifu, Yeye yuko kwenye wakati mzuri kabisa.

<sup>126</sup> Mkutano huu si wa majaliwa, ni njia iliyoandaliwa na Mungu kwa ajili yetu, uko tu katika msimu ufaao, wakati ufaao. Hukuja hapa alasiri ya leo kwa bahati tu, Mungu ndiye aliyekuleta hapa. Kila kitu kinasonga vizuri kabisa. Sasa, kama unataka kusikiliza, kama unataka kuamini, hilo litakuwa

juu yako, lakini kwenye ile Hukumu, basi Mungu atasema, “Unakumbuka?” Uh-huh. Basi unaweza kusema nini?

127 Sasa, angalieni, basi nilivutiwa.. Hili linasikika sana sana kama mzaha mdogo, bali sio mzaha. Basi nilipokuwa nikiuzunguka huo mti mbio ndipo ghafla maskini kuchakulo mdogo wa misonobari. . . Sijui kama mnao huku juu ama hamna. Ye—yeye ndiye maskini kitu chenye kelele kuliko vyote vilivyoko mwituni, ananinii tu, vema, ni kama tu wasemavyo, bundi wa Mwairishi, kelele tupu na manyoya wala hamna bundi.

Kwa hiyo ye—yeye alikuwa tu. . . anabweka tu na kupiga makelele. Bw. Jeverez alizoea kuniambia. . . Nilisema, “Ni kitu gani kinachowafanya wapige makelele?”

Akasema, “Anakulaani.”

Nikasema, “*Tsk, tsk, tsk, tsk, tsk*, lugha kama hiyo!”

128 Na wakati a—alipokuwa akipiga makelele, akirukaruka tu juu chini. Nami nikawazia, “Kwa nini umesisimkwa sana, ewe jamaa mdogo?” Nikasema, “Kwani nilikulisimua, kwa sababu nilikuwa nikikimbia kuuzunguka huu mti? Angalia hili!” Ndipo nikazunguka na kuzunguka tena.

129 Naye alikuwa tu ameketi pale, akipayuka-payuka tu juu ya ki—kisiki ambapo mti ulikuwa umeanguka. Nami nikasema, “Je, ulijua ninamwabudu Mungu yeye yule aliyekuumba?” Sasa, nilisema. . .

130 Nikazunguka mbio mara kadhaa zaidi, ndipo nikamwona maskini jamaa huyo, nilifikiri nilikuwa nimemsisimua, bali alikuwa ametokeza jicho lake dogo shavuni mwake, naye alikuwa akiangalia chini kwenye huo uwazi. Nami nikawaza, “Vema, kuna nini huko chini?” Kumbema dhoruba ilikuwa imemshusha chini tai mkubwa, na huyo ndiye aliyekuwa akimbwekea, si mimi, ilikuwa ni yule tai.

131 Kwa hiyo nikaangalia ndipo tai huyu mkubwa akaruka juu. Huko Colorado tuna tai wa hudhurungi, ndege mkubwa mno anayependeza. Nami ninawapenda tai, kwa sababu Mungu huwafananisha watoto Wake, urithi Wake, na tai, naye Mungu, Mwenyewe, anajiita Tai, Yeye ni Yehova Tai, Bapa Tai, sisi ni vifaranga vya tai Wake.

132 Tai anaweza kuruka juu zaidi kuliko ndege mwingine yeyote aliyepo. Kama mwewe angejaribu kumfuata, angechanganukia hewani, kwa hiyo ukijaribu kuiga Ukristo, unajipasua tu wazi, hivyo tu, haikufai chochote. Kuwa tai, uzaliwe mara ya pili, maumbile yabadilishwe, ndipo unaweza kupanda ngazi ya Yakobo, ndipo unaweza kupanda hadi mahali pa juu sana ambapo mambo yote yanawezekana kwa hao waaminio, bali huna budi kuwa tai, mwaminio.

133 Usijaribu. . . Waebrania walipovuka, kama tai, wakavuka Bahari ya Shamu, kule kupima, wakifuatilia, Wamisri

wasiotahiriwa walijaribu kufanya hivyo nao wakapoteza maisha yao. Huwezi kuiga Ukristo, huna budi kuwa Mkristo. Hiyo ni kweli.

<sup>134</sup> Sasa, nilikuwa nimemwona jamaa huyu mkubwa, nami ni—nikaacha kupiga makelele au kuzunguka-zunguka mti kwa mhemko, na—nami nikamwangalia tai huyu mkubwa, ndipo nikasema, “Sasa, sijui ni kwa nini Mungu alinikomesha kupiga makelele?” Ninaamini ya kwamba kila kitu hufanya kazi pamoja kwa manufaa. Nami nikawazia, “Nilikuwa na wakati mzuri sana, kwa nini unikomeshe sasa kumtazama huyo tai? Maskini mla mizoga!” Nikasema, “Vema, kile—kile—kile Wewe . . . ? Sioni kitu chochote cha kijasiri juu yake, cha kiungu sana.”

<sup>135</sup> Lakini nikawazia, “Kila kitu huku juu hakina budi kuwa na Mungu ndani yake.” Kila kitu, unaweza kumtazama mtu mbaya kuliko wote duniani na utapata mambo mazuri kumhusu. Hiyo ni kweli. Kwa hiyo Mungu yuko kila mahali, inakubidi tu kuangalia kila mahali umpate.

<sup>136</sup> Hiyo ndiyo sababu Yesu alisema . . . Nami naamini kama una mtu . . . Unaweza kumpenda mtu yeyote anayekupenda, lakini je, unaweza kuwapenda wale wasiokupenda? Huyu ni Roho wa Kristo. Mnaona? Wakati hao watakapokutenda mabaya na kusema maovu dhidi yako na kutoka moyoni mwako ungali unawapenda, basi unajua unakaribia Ufalme basi. Unaona? Kwa hiyo akasema, “Tukiwapenda wale wanaotupenda tu, tuna thawabu gani?”

<sup>137</sup> Kwa hiyo nikamwangalia maskini huyo tai nami nikaona hayo macho makubwa ya kijivu, yalipokuwa yakipepesa. Ndipo nikawazia, “Vema, ni nini . . . ? Ningeweza kuona kitu gani cha kiungu kuhusu jamaa huyo? Yeye ni sehemu ya maumbile. Vema, ningeweza kuona kitu gani cha kiungu kwake?” Niliona yeye hakuogopa, na huyo ni Mungu pale, peke yake.

<sup>138</sup> Mungu hana haja na mtu mwoga. Kama unaogopa kumwamini, hata usijaribu, mpaka utakaporidhika ya kwamba Yeye hutimiza Neno Lake na hutimiza ahadi Yake, basi hakuna kitu kitakachokuzuia. Hiyo ni kweli. Lakini hakikisha unajua mahali unaposimama, kwa sababu utajifanya tu kuwa mbaya zaidi.

<sup>139</sup> Ndipo nikamwona, nikawazia, “Hivi huniogopi mimi?” Nilikuwa nimeegemeza bunduki yangu kwenye mti, nikasema, “Ninaweza kunyakua bunduki yangu na kukupiga risasi.” Naye akaketi tu pale, ndipo nikaona, “Nini . . . ? Kumbé, yeye . . . ? Kwa nini haogopi?” Nami nikaona kwamba alikuwa na mabawa yake, akaendelea kuyapapasa, aone kama manyoya yote yalikuwa sawa.

<sup>140</sup> Nikawazia, “Jambo ndilo hilo! Mungu amempa mabawa mawili, ana imani nayo. Anajua ya kwamba angeweza kuingia kwenye msitu huo kabla sijaishika bunduki hiyo, naye ana

imani kamilifu katika njia yake ya kutoroka aliyopewa na Mungu.” Na kama tai, katika ulimwengu wa Mungu, anaweza kuamini vya kutosha kipawa alichopewa na Mungu cha mabawa yake, ni zaidi sana vipi sisi, watoto wa Mungu, tunavyopaswa kumwamini Roho Mtakatifu, hata ingawa daktari anasema utakufa kwa kansa, mradi tu unaweza kuhisi nguvu hizo za Mungu hapo, acha kila kitu kiwe uongo na Neno la Mungu liwe kweli.

<sup>141</sup> Nilimwalia, nikawaza, “Haya basi Mungu, ninakuona Wewe sasa, kwa sababu yeye haogopi.” Mungu anamchukia mwoga. Upendo huitupilia mbali hofu, kwa hiyo kama una upendo, huna hofu yoyote. Hakuna kitu... Hofu haina hata chembe moja ya thamani kwake, hakuna kitu kimoja, itakuzuia.

<sup>142</sup> Unasema, “Vema, vipi kama utapigwa risasi asubuhi? Hivi hungeogopa?” La, bwana. Hofu isingeweza kunisaidia, hofu ingeweza tu kunifanyia hali mbaya zaidi. “Vema, imani ingeweza kukusaidia nini kama tayari wametia sahihi ya kwamba utakufa asubuhi?” Imani inaweza kutia sahihi msamaha wangu. Amina. Kwa hiyo acha nichukue imani.

<sup>143</sup> Kama daktari akisema utakufa kwa kansa, hayo tu ndiyo ajuayo, amini, nayo itakubadilishia hali ya mambo. Kama akisema hutatembea tena, huyo mtu anasema kweli, hayo tu ndiyo ajuayo. Hayo tu ndiyo anayoweza kuangalia, yale anayoweza... Anaweza tu kufuata hisia zake: kugusa, kunusa, kuonja, kusikia. Lakini unaona, imani ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo, ni bayana ya mambo usiyohisi, kuonja, kunusa, wala kusikia. Ni imani, unaiamini, ni hisi ya sita, imepita zile hisi tano.

<sup>144</sup> Ndipo nikamwalia jamaa huyo, nikawaza, “Loo, ninakupenda sana.” Nikasema, “Mungu, ninakuona katika huyo tai.” Naye akaniangalia kwa muda kidogo, akagundua kwamba nilikuwa rafiki yake, kwa hiyo sikuwa ninaenda kumdhuru.

<sup>145</sup> Basi baada ya kitambo kidogo, akaendelea kumwalia huyo kuchakulo wa misonobari, basi nikaona kwamba kuchakulo huyo wa misonobari alikuwa—alikuwa ndiye aliyekuwa akimlaani sana. Naye akachoshwa na hayo, kwa hiyo akainama tu chini na kufanya kishindo kikubwa kwa mbawa zake, yapata vishindo viwili akaupita huo msitu. Basi nikaona alilofanya, kamwe sitalisahau.

<sup>146</sup> Sikilizeni, eni wategaji, wawindaji, yeye alijua jinsi ya kuweka mabawa yake. Basi kulikuwa na upepo mwanana uliovuma mlimani, kila wakati huo upepo mwanana ungekuja, angepanda tu juu yake, upepo mwingine mwanana ungekuja, angepanda juu zaidi kidogo, kisha upepo mwingine mwanana ungekuja, angeenda juu zaidi kidogo, kamwe hakusogeza unyoya, alijua tu jinsi ya kutega mabawa yake.

147 Nami nikasimama na kumwanguka mpaka akatoweka kabisa. Nikasimama pale huku machozi yakitiririka mashavuni mwangu. Nikasema, “Hilo ndilo, Mungu, wazo ndilo hilo. Si . . .” [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . naye akaruka akaenda zake. Ee Mungu! Jambo ndilo hilo.

148 Jua tu jinsi ya kuweka tumaini lako katika Neno Lake na kusema ni la kweli. “Mungu Katika Ulimwengu Wake.” Mnaamini Yeye yuko katika ulimwengu Wake? Yeye yuko katika maua Yake. Hivi mnaweza kumwona sasa, kile ninachomaanisha, katika kutua kwa jua, kuchomoza kwa jua, katika kuishikilia dunia, kuzunguka kwa mfumo wa jua, yote aliyo Yeye? Ningeweza kuchukua saa, saa kadhaa, kwenye somo hilo moja tu, “Mungu Katika Ulimwengu Wake.”

149 Hebu niwaambieni, ninaamini mnapata gazeti karibu mara mbili kwa juma hapa Dawson, sivyo? Sasa, hebu watangazaji wa habari waseme kesho, majira ya majani kupukutika mwakani yanakaribia, naye atasema, “Kesho kutakuwa na hali nzuri ya hewa, kutakuwa shwari na joto kesho.” Nawe umwone maskini nguruwe huyo akitoa hayo makapi kutoka upande wa kaskazini wa hicho kilima, na kuyaleta upande wa kusini wa kilima, anajua zaidi kuhusu hali hiyo ya hewa kuliko watabiri wote ulimwenguni, wewe itazamie hali baridi ya hewa.

150 Ukiwaona hao sungura wakirudi nyuma kabisa vichakani, naye mwandishi wa habari aseme, “Hali ya hewa itakuwa nzuri,” usiamini hilo, mvua inakaribia. Unaona? Anajua zaidi kulihusu kuliko watangazaji wote wa habari wajuavyo, kwa sababu ana silika aliyopewa na Mungu. Yeye ni sehemu ya ulimwengu wa Mungu. “Mungu Katika Ulimwengu Wake.”

151 Sasa, “Mungu Katika Neno Lake.” Sasa, nitajaribu kuharakisha ili tuweze kuharakisha, ninachelewa. Hiyo ndiyo shida yangu, ninaongea kupita kiasi, ninawaweka muda mrefu sana. Ila maharagwe hayataungua, na yakiungua, tutongezea mengine. Sasa, hiki ndicho—hiki ndicho Chakula mnachohitaji kwa ajili ya Uzima wa Milele.

152 “Mungu katika Neno Lake.” Sasa, Biblia ilisema ya kwamba Neno la Mungu ni Mbegu ambayo mpanzi alipanda. Sasa, tunajua, ninyi wakulima hapa, je, mnajua ya kwamba unapopanda mbegu, kama ukipanda ngano, mbona, itazaa ngano, kama ikitunzwa vizuri. Ukipanda shayiri, itazaa shayiri, ikitunzwa vizuri. Vema, hivyo ndivyo Neno la Mungu lilivyo: Ukichukua ahadi yoyote ya Mungu na kuiweka katika mazingira mazuri, itazaa jinsi ilivyo hasa katika Maisha yake.

153 Kama vile kuku, kwa kawaida, utaratibu mzuri ni kuchukua yai na kuliweka chini ya kuku, naye ataangua kuku. Lakini ungeweza kuchukua ya—yai, mazingira ndiyo muhimu, chukua yai lilo hilo la kuku na kuliweka chini ya m—mtoto wa mbwa, na

kuuacha mwili wa huyo mbwa uendeleo kulipasha hilo yai joto, litaangua kuku. Unaona? Ni mazingira.

<sup>154</sup> Na hilo ndilo jambo lile lile hapa, alasiri ya leo, hilo ndilo ninalozungumzia. Kama tunaweza kupata mazingira mazuri ya Kimbinguni, jambo fulani litatukia, mnaona, mazingira.

<sup>155</sup> Mungu ni . . . Neno ni Mbegu. Sasa, hebu chukua mti mdogo, kama ninii mdogo, chukua, wengi wenu ninyi watu mna bustani, hebu chukua mtofaa mdogo, sasa, angalieni jambo hili, hebu chukua maskini mtofaa huo kama chipukizi, ni karibu ukubwa *huo* tu, inatoka kwenye mbegu. Vema, hivi ulijua kila tofaa litakalowahi kuwa kwenye mti huo liko ndani yake papo hapo? Ulijua hilo?

<sup>156</sup> Unasema, “Mti huo utazaa matofaa mangapi?” Labda pishi mia moja na hamsini, pishi mia mbili, pishi mia tano katika maisha ya huo mti. Lakini sasa, pishi zote mia tano za matofaa ziko ndani yake wakati ukiwa tu yapata ukubwa *huo*. Kama sivyo, naomba, niambiieni yanatoka wapi? Mnaona? Yako ndani yake.

<sup>157</sup> Sasa, unafanya nini na huo mti? Hebu utoe, uweke chini ardhini, na kuupanda, kisha uutie maji. Sasa, huo mti mdogo unapaswa kufanya nini? Mti huo mdogo hauna budi kunywa maji kutoka ardhini, nao hauna budi kunywa, na kunywa, na kunywa, hauna budi kunywa zaidi ya kipimo chake. Nao unapokunywa, unaanza kusukuma nje, na baada ya kitambo kidogo, unasukuma nje matawi, kisha unasukuma nje majani, kisha unasukuma nje maua, kisha unasukuma nje matofaa. Ni kunywa tu na kusukuma.

<sup>158</sup> Na hivyo ndivyo Mkristo alivyo. Tumepandwa katika Kristo Yesu, ambaye, kwa tafsiri yangu, ndiye Chemchemi ya Uzima isiyomalizika. Na jambo pekee tunalopaswa kufanya, kama wewe ni mgonjwa, kama unahitaji kitu fulani, wakati Mungu anapokujaza na Roho Mtakatifu, wewe ni, kwa Roho mmoja sisi sote tumepandwa, tumebatizwa kuwa Mwili mmoja, na jambo pekee tunalopaswa kufanya basi ni kunywa tu, kunywa, mpaka tutakapousukuma nje uponyaji wa Kiungu, utukufu, na kuondolea mbali wasiwasi wa kale na mashaka, na kuyasukumia mbali, na kuingiza Uzima mpya, tuzae matunda mapya ya Roho. Kunywa tu, kunywa; ile Mbegu.

<sup>159</sup> Nilikuwa pamoja na Bw. Durney. Baadhi ya watu wangu hapa watajua ya kwamba nimewaambia jambo hili. Tulipanda mlimani kumchukua mbuzi, ndipo tulipokuwa tukishuka, tulipitia mahali pa—palipounguzwa moto pa kale ama kitu fulani. Nami. . . Kuhusu dubu niliyekuwa nimemwona kule chini, nadhani unamkumbuka, Bw. Durney, maskini yule dubu, nikasema, “Ngozi yake ni nzito sana hatuwezi kuibeba mpaka chini ya ule mlima.”

<sup>160</sup> Nami nilikuwa nikimwangalia usoni, nami nilikuwa kidogo ninachoka. Kwa hiyo ilipoelekea kuingia giza usiku huo, niliona tulifikia mahali ambapo huko kuunguzwa kulikuwa kumeacha vi—visiki vichache vimesimama, navyo vilikuwa vimebanduka tu viwezavyo kuwa.

<sup>161</sup> Nasi tulikuwa tukipumzika kidogo, ba—basi nikawazia pale kwamba... akiwaendea wale farasi, nao upepo ukavuma, ndipo upepo ulipovuma, sauti ya kutisha sana ikasikika, “Uuum!” Nikawazia, “Jamani, vinaonekana kama mawe ya makaburi, hapa ni mahali pa kudhoofisha.” Nami nikawaza, “Baba, ni kitu gani hiki?”

Inanikumbusha juu ya mtu fulani akijaribu... Nitasema, “Je, wewe ni Mkristo?”

“Mimi ni Mpresbiteri.” “Mimi ni Mbaptisti.” “Mimi ni Mmethodisti.”

<sup>162</sup> Mnajua ni nini? Ni wewe ukijaribu kushikilia na kuingia Mbinguni kwa kuwa mfuasi wa dhehebu fulani. Sasa, dhehebu hilo ni sawa, lakini kumbukeni, kila wakati dhehebu linapochipuka, Mungu huliacha. Huendi Mbinguni kwa dhehebu, unaenda Mbinguni kwa Mbegu hii mpya ya Mungu kuzaliwa moyoni mwako. Hiyo ni kweli.

<sup>163</sup> Basi nilisikia kelele hizo za maombolezi, nami nikasema, “Hapa ni mahali panapochosha kuwepo, natumaini hatutawasha moto na kukaa hapa.” Nao mwezi ulikuwa umechomoza, na hiyo miti ya kale iliyometameta namna hiyo, nikawaza, “Hilo si ni jambo la kuchukiza sana?” Mahali pa kale, panapoonekana kama mawe ya makaburi, panachosha. Vilikuwa vikisema nini? “Wakati mmoja tulikuwa misonobari mikubwa, inayoyumbayumba, lakini moto ukatuteketeza.”

<sup>164</sup> Na hivyo ndivyo ilivyo siku hizi. Ninapouliza, “Je, wewe ni Mkristo?” hawajui maana ya kuwa Mkristo, watu wengi.

Wanasema, “Loo, mimi ni Mmethodisti.” “Mimi ni Mbaptisti.” “Mimi ni Mpentekoste.” “Mimi ni Mpresbiteri.”

<sup>165</sup> Hilo halina uhusiano wowote nalo. Isipokuwa maskini Mbegu hiyo imeingia hapa ndani, basi unaweza kuwa mfuasi wa chochote unachotaka kuwa, wewe ni Mkristo aliyezaliwa mara ya pili basi, lakini bila hiyo, umepotea. Mungu ni Mbegu, Neno Lake ni Mbegu.

<sup>166</sup> Niliona jambo lingine, Bw. Durney, Chris, ambalo niliona maskini misonobari hiyo. Nikawazia, “Vema sasa, hayo ni yale madhehebu makubwa mno, kasema, ‘Loo, wakati mmoja tulikuwa na John Wesley. Wakati mmoja tulikuwa na Martin Luther. Wakati mmoja tulikuwa na Sankey, Finney, Knox, Calvin.’” Hiyo ni kweli. Lakini mnaona mlicho nacho sasa?

<sup>167</sup> Hao watu walimwamini Mungu, wakafanya uponyaji wa Kiungu na kila namna ya miujiza. Hiyo ni kweli. Lakini sasa,



mna nini? Madhehebu yenye upepo dhaifu ukivuma. Kila wakati Mungu anaposhusha upepo wenye nguvu ukienda kasi, kama alivyofanya kwenye Siku ya Pentekoste, mnajua mnachosema? “*Uuum!* Msiuendee huo, ni wa ibilisi. *Uuuu!* Siku za miujiza zimepita. Hakuna kitu kama uponyaji wa Kiungu. *Uuum!* Tunayo yameandikwa kwenye kanuni zetu za imani, ‘Hakuna kitu kama uponyaji wa Kiungu.’” Wamekufa, hawawezi... hawawezi kubadilisha mawazo.

<sup>168</sup> Sasa, niliona basi, chini ya hiyo, kulikuwa na mbegu zilizopukutika kutoka kwenye misonobari hiyo. Na kama uliwahi kuichunguza misonobari, njia pekee inayoweza kujizalisha ni joto hilo kushuka na kuifungua sonobari hiyo na kuacha mbegu iingie ardhini, ndipo kinakuja kizazi kipya, mti mwingine. Ndipo upepo ulipovuma, hao jamaa wadogo hawakuguna, walichezacheza tu katika upepo.

<sup>169</sup> Nikawaza, “Vema, Yeye anapuliza upepo kwa sababu gani?” Vema, mnaona, kila wakati upepo unapovuma, unausogeza huo mti mdogo, nao unaivuta mizizi, unailegeza ili iweze kushuka chini na kushikilia imara zaidi. Ndipo nikawaza, “Jambo ndilo hilo, Bwana!” Nikawaza, “Bw. Durney atafikiri nina kichaa, lakini ninajisikia kuruka juu kwenye moja ya matawi haya hapa na kukimbia huku na huko hapa, kama mmoja wa hao kuchakulo, nikipiga mayowe kwa sauti yangu yote.” Jambo ndilo hilo.

<sup>170</sup> “Wakati mmoja tulikuwa na Kanisa lililoamini katika uponyaji wa Kiungu.” “Wakati mmoja tulikuwa na Martin Luther.” “Wakati mmoja tulikuwa na John Wesley.” Lakini sasa, ninyi ni nini? Sanamu iliyokufa.

<sup>171</sup> Lakini chini ya hayo yote, Jina la Mungu libarikiwe, tungali tuna Mbegu ya Mungu ambayo imezaa Kanisa lingine. Kitu fulani kimezaa Kanisa linaloamini ya kwamba Mungu ni Mungu aliye hai, na wakati Mungu anaposhusha huo Upepo wa Kipentekoste, unaoenda kasi, wanayumbayumba tu na kucheza ndani Yake. Unasema, “Wao ni wa kijani kibichi.” Lakini wana wakati mzuri, nao wanakua. Kama wao ni wa kijani kibichi, wana Uhai. Kama wewe si kijani kibichi kidogo, mbona, huna Uhai wowote.

<sup>172</sup> Maskini Mnorwe, hapa si muda mrefu uliopita, aliingia na kuokoka mkutanoni. Akarudi kwa bosu wake, akasema, “Loo, *Dori* kwa *Dodi*.” Akasema, “Bwana asifiwe, tayari *nimebata Roho Mdagadifu*.”

Bosu wake akasema, “Ati unasema nini?”

Akasema, “Ni—nilishuka kwenda kanisani na,” kasema kwamba “Mungu alinipa Roho Mtakatifu. *Msuru, msuri, msuri* sana najisikia.”

Akasema, “Hapana shaka wewe ni mfuasi wa kundi hilo la nati kule chini.”

173 Akasema, “Mungu asifiwe kwa ajili ya nati.” Akasema, “Unajua nini?” Kasema, “Kama ni . . . Hebu chukua tuseme motokaa, kama haikuwa na nati zozote ndani yake, ingekuwa ni lundo kubwa la *vikorokoro*.”

174 Hiyo ndiyo njia! Kama hatuwezi kuwa na mtu humu ndani aliye na nguvu za kutosha, na uweza wa kutosha, na kumwamini Mungu vya kutosha kushikilia kitu hicho pamoja, tuna nini ila vikorokoro vikubwa vya kimadhehebu! Kweli. Mungu asifiwe kwa ajili ya nati zinazoshikilia kitu hicho pamoja.

175 Kama nilivyowahubiria jana usiku, mtu anapompokea Roho Mtakatifu yeye hutenda kiwazimu hata hivyo. Lakini yeye anatenda hilo tu kwa watu wa ulimwengu, kwa Mungu. . . Yeye ni Baba mtukufu.

176 Mwangalieni Daudi wakati alipocheza kuzunguka lile sanduku, naye mke wake aliyeketi pale juu, kasema, “Unaniaibisha, ma—malkia.” Kwa maneno mengine, yeye. . . “Mi—mimi ni binti wa mfalme, nawe ulikuwa huko nje na kukimbia-kimbia, ukipiga mayowe karibu na hilo sanduku, ukicheza namna hiyo!”

Daudi akasema, “Kumbe hukupendezwa na hiyo? Angalia hii!” Ndipo akazunguka, akazunguka tena, akacheza dansi karibu na hapo, kasema, “Angalia hiyo.”

177 Ndipo Mungu akaangalia chini kutoka Mbinguni na kusema, “Daudi, wewe ni mtu anayeupendeza moyo Wangu.” Sasa, inategemea wewe ni wa moyo wa nani. Kama wewe ni wa moyo wa ulimwengu, utatenda kama ulimwengu, lakini kama wewe ni wa moyo wa Mungu, utafanya mambo ambayo ulimwengu haujui kitu kuyahusu. Udanganyifu mwingi sana, unaendelea na kuendelea na kuendelea.

178 “Mungu Katika Ulimwengu Wake.” Mnaamini hilo? Mungu yuko katika Neno Lake. Mnaamini hilo? Angalieni jinsi anavyotimiza Neno Lake na kulithibitisha. Angalieni yale aliyowambia Ibrahimu, angalieni yale aliyowaambia mitume, angalieni yale aliyowaambia manabii, angalieni jinsi alivyoahidi katika siku hii. Mungu yuko katika ulimwengu Wake; Mungu yuko katika Neno Lake.

179 Sasa “Mungu Ndani ya Mwanawe.” Mnaamini Mungu alikuwa ndani ya Mwanawe? Sasa, inatubidi kuharakisha. “Mungu alikuwa ndani ya Kristo, akiupatanisha ulimwengu kwa nafsi Yake.” Mnaamini hilo? Tamshi moja juu ya “Mungu Ndani ya Mwanawe,” ili tuweze kuharakisha.

180 Nilikuwa nikizungumza na mwanamke mmoja, si muda mrefu uliopita, ambaye ni mfuasi wa kanisa ambalo haliamini ya kwamba Yesu alikuwa ni Mungu. Anaamini ya kwamba Yeye alikuwa tu ni mtu wa kawaida, nabii, ama kitu fulani, bali hakuwa Mungu.

181 Ama alikuwa ni Mungu au mdanganyifu mkuu sana ulimwengu umewahi kuwa naye. Yeye alikuwa ni Mungu, Mungu aliyedhihirishwa katika mwili ulioitwa Yesu, Mwanawe, si mwanadamu tu, si mwalimu, mwanafalsafa, bali Yeye alikuwa ni Mungu aliyedhihirishwa katika mwili.

182 Timotheo wa Kwanza 3:16 ilisema, “Bila shaka siri ya utauwa ni kuu, kwa kuwa Mungu alidhihirishwa katika mwili, akaonekana na Malaika, akapokelewa juu Mbinguni.” Vema, hakika, Yeye alikuwa ni Mungu.

Ndipo mama huyu akasema, “Bw. Branham, ninafurahia mahubiri yako, lakini,” akasema, “kuna kosa moja tu ninalopata kwako.”

183 Nikasema, “Asante! Kama unaweza tu kupata kosa moja, hilo ni zuri sana.” Kisha nikasema, “Tayari nimepata milioni elfu kumi yake, labda watu wamepata zaidi ya hayo.” Nikasema, “Iwapo unapata tu moja, na—nakushukuru kwa tamshi hilo.”

Akasema, “Lakini laiti ungelisahihisha hilo.”

Ndipo nikasema, “Ni kitu gani, mama? Naweza kujua? Kama niko karibu hivyo na kuwa ‘sawa,’” Nikasema, “Mimi, labda ninaweza kulisahihisha hilo.”

Akasema, “Unamjivunia Yesu kupita kiasi.” Loo!

Nikasema, “*Ati nini?*”

Akasema, “Unamjivunia Yesu kupita kiasi.”

184 Nikasema, “Nisingeweza kumjivunia vya kutosha, Dada.” Nikasema, “Kama ningalikuwa na lugha elfu kumi, nisingeweza kumsifu vya kutosha. Yeye anastahili sifa zote.”

Akasema, “Lakini unamfanya Mungu.”

“Vema,” nikasema, “Yeye alikuwa ni Mungu.”

Akasema, “Yeye alikuwa ni mwanadamu tu, Bw. Branham. Alikuwa mwalimu mzuri, mwanafalsafa, bali hakuwa Mungu. Unamfanya Mungu.”

Nikasema, “Yeye alikuwa ni Mungu.”

Naye akasema, “Vema, kama nitaninii. . . Ulisema ulikuwa wa kimsingi, ulidumu na Neno.”

Nikasema, “Naam, Mama.”

Akasema, “Kama nitakuonyesha katika Neno ambapo Biblia inaonyesha ya kwamba yeye si Mungu, utakubali?”

Nikasema, “Naam, Mama, lakini huwezi kufanya hivyo. Lakini mimi ni muungwana, Mkristo vya kutosha kukusikiliza.”

185 Naye akasema, “Ninaweza kukuthibitishia.” Kasema, “Hebu chukua Yohana Mtakatifu mlango wa 11.” Kasema, “Wakati Yesu aliposhuka kwenda kumfufua Lazaro, Biblia ilisema alilia.”

Nikasema, “Hakika. Kwa nini?”

“Mbona,” akasema, “hiyo ilionyesha hakuwa Mungu.”

Nikasema, “Hilo ndilo Andiko lako?”

Akasema, “Naam, hilo Ndilo.”

<sup>186</sup> Nikasema, “Dada, hayo ni membamba kuliko mchuzi uliotengenezwa kwa kivuli cha kuku aliyekufa kwa njaa.” Nikasema, “Kama hayo ndiyo yote uliyo nayo! Jamani! Loo,” nikasema, “hivi huelewi? Alikuwa Mungu na mwanadamu pia, Mungu alikuwa ndani Yake.”

Naye akasema, “Angewezaje kulia kama alikuwa ni Mungu?”

<sup>187</sup> Nikasema, “Vema, hebu tuendelee na hilo somo. Nitakubali ya kwamba Yeye alikuwa ni Mwanadamu, ila alikuwa Mungu-Mwanadamu.” Nikasema, “Alienda kwenye kaburi la Lazaro, akalia kama mwanadamu. Lakini aliposimama pale na kuyavuta hayo mabega madogo pamoja, ‘Lazaro, njoo huku,’ naye mtu, aliyekuwa amekufa siku nne, pua yake tayari ilikuwa imebonyea ndani, mabuu ya ngozi yakila mwilini mwake, nafsi yake ilikuwa kwenye safari ya siku nne mahali fulani. . .

<sup>188</sup> “Sijui, wala siamini nyinyi mnajua pia, lakini nafsi yake ilikuwa imeondoka siku nne, mwili wake, uharibifu ulikuwa umeingia, Naye akasema, ‘Lazaro, njoo huku,’ na mtu aliyekuwa amekufa siku nne akasimama kwa miguu yake akaishi tena.” Ndugu, huyo alikuwa ni zaidi ya mwanadamu kufanya hivyo, huyo alikuwa ni Mungu ndani ya Mwanadamu.

<sup>189</sup> Hakika, Yeye alikuwa ni Mwanadamu wakati aliposhuka kutoka mlimani siku hiyo, akiwa na njaa, akiangalia kote kwenye miti apate tini ale, aliona njaa; alikuwa na njaa kama mwanadamu. Lakini alipochukua biskuti tano ndogo na samaki wawili na kuwalisha watu elfu tano, huyo alikuwa ni zaidi ya mwanadamu, huyo alikuwa ni Mungu ndani ya Mwanadamu ambaye angeweza kuumega mkate huo na kuzidisha mikate na kupika samaki, kuitoa. Hiyo ni kweli. Alikuwa zaidi ya mwanadamu.

<sup>190</sup> Pia ni kweli, Yeye alikuwa ni Mwanadamu wakati alipokuwa amelala huko nje kwenye mashua hiyo usiku huo, dhoruba hiyo ikatokea, pepo elfu kumi wa baharini wakaapa wangemzamisha, alikuwa amechoka sana kutokana na kuona maono na kuwaombea wagonjwa. Ndipo maskini mtumbwi huo mdogo, kama kifuniko cha chupa huko nje, ukirushwa-rushwa, huku ibilisi anasema, “Tumempata sasa, amelala.”

<sup>191</sup> Yeye alikuwa ni Mwanadamu wakati alipokuwa amechoka, akilala, lakini alipouweka mguu Wake kwenye demani ya hicho chombo na kuangalia juu na kusema, “Amani, tulia,” na pepo na mawimbi yakamtii, huyo alikuwa ni zaidi ya mwanadamu, huyo alikuwa ni Mungu akinena kupitia Mtu huyo.

<sup>192</sup> Alikuwa Mwanadamu wakati alipolia pale Kalvari, “Mungu Wangu, mbona umeniacha?” Alikuwa ni Mwanadamu wakati

alipokuwa akililia rehema, lakini katika siku hiyo ya tatu, wakati alipovunja mihuri ya mauti, kuzimu, na kaburi, na kufufuka, alithibitisha Yeye alikuwa ni Mungu.

<sup>193</sup> Si ajabu washairi...Imevuvia maisha ya kila mshairi ama kila mwandishi aliyewahi kuandika wimbo. Mtu yeyote aliyepata kuwa na thamani yoyote aliamini hiyo kuwa ni kweli.

Eddie Perronet, alipokuwa katika wakati wake mkuu, nao walikuwa wakimtesa, aliandika wimbo:

Nyote zisifuni nguvu za Jina la Yesu!  
Malaika na wasujudu;  
Leteni taji ya kifalme,  
Na kumvika taji Bwana wa wote.

Mwingine mmoja aliandika:

Nyote zisifuni nguvu za Jina la Yesu!  
Malaika na wasujudu;

Loo, jamani! Ungeweza je...?

Juu ya Kristo, Mwamba imara, ninasimama;  
Sakafu zingine zote ni mchanga udidimiao.

Ningesema nini? Maskini kipofu Fanny Crosby, uliwazia nini juu yake? Alisema:

Usinipite, Ee Mwokozi mpole,  
Sikia kilio changu kinyenyekevu;  
Unapowazuru wengine,  
Usinipite.

Kwa kuwa Wewe ni Kijito cha faraja yangu  
yote,  
U zaidi ya uhai kwangu,  
Ni nani niliye naye duniani ila Wewe?  
Au ni nani Mbinguni ila Wewe?

Na iwe chochote kile, Kerubi, ama kijimungu fulani, “Ni nani Mbinguni ila Wewe?”

Kisha mmoja akasema:

Alipoishi, alinipenda; akifa, Yeye aliniokoa;  
Alipozikwa, alizipeleka dhambi zangu mbali  
sana;  
Alipofufuka, alinihesabia haki bure milele:  
Siku moja Yeye yuaja—loo, siku yenye utukufu!

Ndilo tumaini la Kanisa: Mungu katika Mwanawe, akiupatanisha ulimwengu kwa nafsi Yake.

<sup>194</sup> Mnaamini Mungu yuko katika ulimwengu Wake? Mungu yuko katika Neno Lake; Mungu yuko ndani ya Mwanawe. Sasa, “Mungu Katika Watu Wake,” nasi tutaninii... tukifunga.

Je, mnaweza kumwona katika ulimwengu Wake? Kumwona katika Neno Lake? Kumwona katika Mwanawe? Sasa, hebu tumwangelie katika watu Wake.

<sup>195</sup> Mungu hukaa pamoja na watu Wake, baada ya wao kufa Yeye angali pamoja nao. Kulikuwa na mzee, mwenye umri wa kama miaka themanini, ambaye alikuwa na sehemu maradufu juu yake, jina lake lilikuwa Elisha. Alikuwa na roho ya Eliya, ambayo ilikuwa ni mfano, Eliya Kanisa, na Elisha, ama, Eliya aliye Kristo, na—na Elisha lile Kanisa, akiwa na sehemu maradufu juu yake.

<sup>196</sup> Naye alikuwa amekufa na alikuwa amekufa kwa miaka mingi, nayo mifupa yake ilikuwa imelala kaburini. Nao walikuwa wakimpeleka mtu wakati mmoja kumzika, naye adui alikuwa anakuja, nao wakautupa mwili huu uliokufa juu ya mifupa ya mtu huyo mtauwa, naye akafufuka akawa hai tena.

<sup>197</sup> “Mungu Katika Watu Wake.” Anajua mahali kila mfupa ulipo. Anajua mahali mama amezikwa, anajua mahali baba amezikwa, anajua mahali nyanya na babu wamezikwa. Yeye ni Mungu, Naye yuko ndani ya watu Wake, hakika Yuko.

<sup>198</sup> Kulikuwa na mtu mmoja jina lake Paulo, nao wakachukua kutoka mwilini mwake lesa ama nguo. Mtu mtauwa, ambaye alikuwa nabii wa Bwana, nao watu waliliamini sana, hata wakachukua lesa kutoka mwilini mwake na kuzituma kwa wagonjwa, na pepo wachafu wakawaacha watu. Kutoka kwenye mwili wa mwanadamu! “Mungu ndani ya watu Wake.”

<sup>199</sup> Kulikuwako na maskini mvuvi mmoja, asiye na elimu sana hata asingeweza kuandika jina lake mwenyewe, Biblia ilisema, ni Matendo mlango wa 3, kwamba alikuwa mtu asiye na elimu wala maarifa, jina lake Simoni Petro. Hakuwa na elimu, hata siku moja ya kwenda shuleni. Mungu alikuwa ndani yake sana hata watu wakatambua ya kwamba Mungu alikuwa ndani yake. Walilala katika kivuli chake (Ee Mungu!) nao wakaponywa. “Mungu ndani ya watu Wake.” Mnaamini hilo?

<sup>200</sup> Kulikuwa na watu mia moja na ishirini baada ya kifo Chake, kuzikwa, na kufufuka, wakapanda kwenye chumba cha juu kungojea. Walikuwa waoga, walifunga madirisha. Waliwaogopa Wayahudi, waliogopa kutoa ushuhuda, kwa hiyo wakajificha kwa muda wa siku kumi katika chumba cha juu.

<sup>201</sup> Na kwa ghafla, kukaja sauti kutoka Mbinguni kama upepo wa nguvu ukienda kasi, ukakijaza chumba chote walimokuwa wameketi. Wakafungua madirisha, na kufungua milango, nao hao wakaingia mtaani, wakiihubiri Injili katika lugha zingine. Ilikuwa ni kitu gani? Mungu ndani ya watu Wake.

<sup>202</sup> Yesu alisema, “Bado kitambo kidogo, na ulimwengu hautaniona tena, bali ninyi mtaniona. Kwa sababu Mimi ni hai, ninyi mnaweza kuishi pia. Kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya, nyingi kuliko hizi mtazifanya, maana Mimi naenda

kwa Baba Yangu.” Naye alisema, katika Yohana Mtakatifu 5:19, “Sitendi neno mpaka nimwone Baba akilitenda kwanza.”

<sup>203</sup> Mlikuwa hapa hivi majuzi usiku nilipohubiri juu ya jambo hilo. Yesu, alijitambulishaje Mwenyewe kama Masihi? Kwa sababu angeweza kuyatambua mawazo yao, na kuwaambia shida yao, na yale waliyokuwa wamefanya, na kadhalika namna hiyo, na Biblia inasema dhahiri hiyo ilikuwa ndiyo ishara ya Masihi. “Mungu ndani ya watu Wake.” “Kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya.”

<sup>204</sup> Yule mwanamke, mzinzi, alikuja kisimani kuchota maji, na hapo aliketi Myahudi, akamwambia, “Mwanamke, nipe maji ninywe,” akiwasiliana na roho yake. Nini kilitukia?

“Nipe maji ninywe.”

Naye akasema, “Si kawaida kwenu Wayahudi kutuomba sisi Wasamaria kitu kama hicho.”

<sup>205</sup> Akasema, “Lakini kama ulijua ni Nani ulikuwa unasema naye, ungeniomba Mimi maji unywe.” Nini kilitukia? Aliona shida yake, sote tunajua ilikuwa ni nini. Kasema, “Nenda, kamwite mumeo, mje naye hapa.”

Akasema, “Sina mume.”

<sup>206</sup> Akasema, “Kweli umesema kweli. Kwa sababu umekuwa na watano, na yule unayeishi naye sasa siye mume wako.” Sasa, Yeye alisema kweli. Mwanamke alisema nini?

“Naona ya kuwa Wewe ni Nabii. Tunajua ajapo Masihi, Yeye atafanya mambo haya. Lakini u Nani Wewe?”

Akasema, “Mimi ninayesema nawe Ndiye.” Ishara ya Masihi.

<sup>207</sup> Akakimbia mjini na kuwaambia watu wa mjini, “Njoni, mwone Mtu aliyeniambia mimi nilikuwa nani, yale nimefanya. Haimkini Huyu kuwa ndiye Masihi?” Ati nini? Jambo lilo hilo lilitabiriwa kurudi tena Kanisani katika siku za mwisho, kabla tu ya wakati wa mwisho!

<sup>208</sup> Loo, ninajua tuna uigaji wake wa kimwili, ninajua tunao wale wanaoliiga na kujifanya kuwa hivyo, lakini kumbukeni, inahitaji do—dola bandia kufanya iliyo halisi kuangaza vizuri. Nasi hatuna budi kuwa kilicho halisi kabla hapajaweza kuwa na cha bandia. Amina. Jamani, ninajisikia kubarikiwa sasa hivi. Naam, hiyo ni kweli, kwa sababu Mungu yuko ndani ya watu Wake. Mnaamini hilo?

<sup>209</sup> Kama Mungu yuko katika ulimwengu Wake semeni, “Amina.” [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Mungu yuko katika Neno Lake; Mungu yuko ndani ya Mwanawe; Mungu yuko ndani ya watu Wake. Sasa hebu tuone kama ndivyo alivyo. Tunamwona katika ulimwengu Wake, Neno, na kadhalika, hebu tuone kama Yeye yuko ndani ya watu Wake.

210 Nimeahidi kuwaombea watu hapa alasiri ya leo. Sasa, mimi kuomba huenda kukawasaidia, ninaunganisha tu imani yangu pamoja na yenu. Lakini, ndugu yangu, mpaka uamini ya kwamba Mungu yuko hapa ndani ya watu Wake, mpaka unapoweza kumwona Mungu yeye yule ambaye tumenena habari zake akijidhihirisha Mwenyewe papa hapa miongoni mwa watu Wake. . .

211 Angefanyaje jambo hilo kama angekuja hapa? Kama Yesu angalisimama hapa alasiri ya leo amevaa suti hii aliyonipa, nawe ungemwendea na kusema, “Bwana Yesu, mimi ni mgonjwa. Utaniponya?” Unajua maneno Yake yangekuwaje? “Tayari nimefanya hivyo, mwanangu.” Alifanya hivyo pale Kalvari. Ni wangapi wanaojua hilo kuwa ni kweli? Ni kweli. Alifanya hivyo pale Kalvari.

212 Basi angefanya nini? Angesema, “Hivi huwezi kuamini nilijeruhiwa kwa makosa yako, na kwa mapigo Yangu wewe uliponya?” Sasa, Yeye angeweza kuthibitisha ya kwamba Yeye alikuwa ni Bwana Yesu, angeweza kufanya hivyo. Angefanyaje jambo hilo? Kwa kuonyesha Yeye alikuwa ni Masihi. Yeye alikuwa ni Bwana.

213 Walijuaaje katika siku hizo, Yeye alikuwa ni Bwana? Kwa sababu alionyesha ishara ya nabii na kila mtu akaamini ya kwamba alikuwa Ndiye. Sasa, haijakuwapo kwa miaka elfu mbili, mpaka siku hii ya mwisho tunayoishi, nasi tunajua jambo hilo.

214 Sasa, kama Yesu atakuja alasiri ya leo na kufanya mambo yale yale aliyofanya alipokuwa hapa duniani, mtaamini Yeye yuko miongoni mwa watu Wake na mtamkubali?

Na tuinamishe vichwa vyetu.

215 Bwana mwenye rehema, tunaomba alasiri ya leo sasa. Nimechukua muda mrefu sana, nikizungumza na watu, kwa sababu sijui ni lini nitakapopata hiyo nafasi tena. Sasa, nimelileta hadi umbali huu, Bwana, ya kwamba Wewe uko katika ulimwengu Wako, katika Neno Lako, Wewe uko katika maua Yako, Wewe uko katika uumbaji Wako, Wewe uko ndani ya Mwanao, na sasa, nimeileta kwa watu Wako.

216 Na sasa, Baba, siwezi kwenda mbali zaidi ya hapa, inakuhitaji Wewe tangu sasa na kuendelea. Ninaomba ya kwamba utasaidia na utalithibitisha Neno Lako kwa ishara zinazofuata, kusudi watu hawa wapate kujua ya kwamba Wewe ni Kristo, ya kwamba Wewe ni Mwana wa Mungu, nasi ni watumishi Wako.

217 Na iwapo kunaweza kuwa mtu hapa ambaye si mwaminio, jalia wakukubali Wewe kama Mwokozi wao binafsi. Kama kuna wale hapa ambao ndio kwanza wajiunge na kanisa wala hawajui maana ya kuwa katika Uwepo wa Kristo Aliye Hai mchana na usiku, jalia walikubali alasiri ya leo.



218 Mponye kila mtu aliyepo, Bwana. Hakika, kama Mungu yuyu huyu ambaye nimezungumza habari zake anaweza kujionyesha Mwenyewe ya kwamba yu hai hapa, nasi tunawaona wahusika wa Biblia . . .

Maisha ya watu mashuhuri yote  
yanatukumbusha, (alisema mshairi,  
Tunaweza kufanya maisha yetu adhimu,  
Tunapoachana, tunaacha nyuma yetu  
Kumbukumbu za kudumu.

Kumbukumbu ambazo labda mwingine,  
Wakati akisafiri juu ya bahari kuu ya maisha,  
Basi ndugu mnyonge na aliyeharibikiwa na  
chombo,  
Akiona, atatiwa moyo tena.

219 Ee Mungu, jalia tuwe watumishi Wako alasiri ya leo. Njoo sasa, Baba. Tunakuona katika ulimwengu Wako, na katika Neno Lako, katika Mwanao, sasa njoo ujithibitisha Mwenyewe kuwa hai miongoni mwa watu.

220 Ndipo tutakapoondoka kwenye jengo hili leo, kwenda kwenye makazi yetu mbalimbali, jalia ninii yetu . . . tuseme kama wale waliotoka Emau. Walikuwa wametembea pamoja Nawe siku nzima baada ya kukufuka, bali hawakutambua ilikuwa ni Wewe. Wengi hapa, Bwana, wamekutumikia, Nawe umewaepusha na shida na kadhalika, ninii tu, nao labda hawakutambua ilikuwa ni Wewe.

221 Lakini usiku huo, wakati jua lilipokuwa linatua, kama ilivyo sasa, Ulisimama kwenye nyumba ndogo ya wageni, nao wakakualika ukae pamoja nao. Wao . . . Ulifanya kana kwamba ulitaka kuendelea mbele, ukawapita, lakini wakakushawishi. Basi jalia wanaume na wanawake hapa leo, wafanye jambo lile lile, wakushawishi, "Karibu ukae pamoja nasi, Bwana." Ndipo ulipoingia ndani na kufunga milango, ulifanya jambo kama ulivyofanya kabla ya kusulubiwa Kwako. Walijua ya kwamba Huyu alikuwa ni Bwana Yesu, kwa kuwa hakuna mtu angaliweza kufanya kama Yeye alivyofanya.

222 Sasa, Baba, ninaomba, ya kwamba katika Jina la Yesu Kristo, ya kwamba Wewe utakuja miongoni mwetu sasa na kuthibitisha ya kwamba mambo haya ambayo nimesema kuhusu Neno Lako, na kukuhusu Wewe ni ya kweli. Jalia tukuone Wewe ukifanya hayo mambo alasiri ya leo, kama ulivyofanya kabla ya kusulubiwa Kwako, ndipo tujue ya kwamba Yesu amefufuka katika wafu na yu hai milele, Naye anaishi miongoni mwa watu Wake.

223 Itawapa watu imani katika watu Wako, Bwana. Itawafanya wanaume na wanawake wayaamini maombi yao na maagizo yao ya jinsi ya kukutana na Wewe. Tujalie, Baba. Tunajikabidhi Kwako pamoja na Neno, katika Jina la Bwana Yesu.

224 Na huku tumeinamisha vichwa vyetu, kungekuwako na wale hapa alasiri ya leo ambao kamwe hawajampokea Kristo kama Mwokozi, kabla hamjaona jambo moja likifanywa, ungesema, “Nikumbuke katika maombi yako, Ndugu Branham, sasa naamini?” [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

225 Hebu mama huyu. . . Njoo tu papa hapa, mama. Sasa, hapa ndipo yote ambayo nimehubiri na yote isemayo Biblia, jambo fulani halina budi kutukia, jambo fulani halina budi kutukia la sivyo Mungu atapatikana kuwa shahidi wa uongo wa Neno Lake Mwenyewe. Mnaona? Hiyo ni kweli.

226 Sasa, kwenu ninyi watu msioamini ya kwamba Yesu ni mkuu tu kadiri alivyowahi kuwa: Sasa, vipi kuhusu hili? Haya hapa mandhari ya Biblia. Ninawatakeni msome Yohana Mtakatifu 4, ambapo mwanamume na mwanamke walikutana kwa mara yao ya kwanza. Tunakutana mara yetu ya kwanza, hiyo ni. . . ? Ili kusanyiko liweze kuona, inua tu mkono wako, kusudi sote wawili. . . Huku Biblia imewekwa hapa, hii ni mara yetu ya kwanza kukutana.

Yuko hapa kwa sababu gani? Ana shida gani? Kwa nini amesimama hapa? Sijui, sijawahi kumwona. Hii ndiyo mara ya kwanza tu kukutana.

227 Sasa, Bw. Durney, nataka uone jambo hili. Niliwaambia kwenye eneo lile la kutegea kwamba Mungu wetu alikuwa ni Mungu. Simama tu papo hapo ulipo kwa dakika moja tu, simama hapo.

228 Huyu hapa mama ambaye sijawahi kumwona maishani mwangu, sijui lolote kuhusu, sijawahi kumwona, ni mgeni kabisa. Sasa, kama Roho Mtakatifu atanifunulia shida ya huyo mwanamke, basi hiyo itabidi itoke kwenye chemchemi fulani ya kiroho, kwa sababu mwanadamu asingejua hilo. Unakumbuka nikiwaambia huko nje kambini mwenu usiku huo?

229 Unakumbuka ule usiku tuliopata zile habari, yule Polisi Mpanda Farasi alinipigia simu, nami sikujua shida ilikuwa ni nini, nilifikiri mvulana wangu alikuwa ameinguka kwenye ndege ama chochote kile, alikuwa shuleni, ndipo usiku huo Bwana akanifunulia ya kwamba hakukuwa na chochote kibaya nyumbani? Hiyo—hiyo ilikuwa huko nyuma kambini mwenu. Sasa, Huyu ni Mungu yeye yule aliye papa hapa sasa. Hii hapa, na mbele zenu.

230 Sijawahi kumwona maishani mwangu. Sasa, kama ninyi watu wote humu ndani mnajua kwamba kwa sa-. . . Mimi, mimi na mwanamke huyu, mbele ya Neno la Mungu, tunaahidi ya kwamba sisi hapa mbele za Mungu, hatujawahi kukutana hapo kabla maishani mwetu.

231 Sasa, huenda akawa ni mgonjwa, huenda akawa na matatizo ya kinyumbani, huenda akawa na matatizo ya kifedha, huenda asiwe sawa na Mungu, huenda akawa ni mtu mwenye sifa mbaya,

huenda yeye ni mtakatifu wa Mungu, sijui lolote kumhusu, yeye amesimama tu hapa.

<sup>232</sup> Sasa, kama hili si jambo lile lile lililotukia katika Yohana Mtakatifu 4, wakati Yesu alipokutana na mwanamke kisimani! Hiyo ni kweli? Ni wangapi watakubali hilo? Hiyo ni kweli.

<sup>233</sup> Sasa, Yesu alimwambia mwanamke huyo shida yake ilikuwa ni nini, naye akasema ilikuwa, hiyo ilikuwa ndiyo ishara ya Masihi. Naye Masihi ni Kristo. Ni wangapi wanaojua hilo? Vema. Basi kama Huyu alikuwa ndiye Masihi jana, naye Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele, halafu mimi, kwa kuwa ni mwanadamu, nisingeweza kumjua, basi itabidi iwe ni Roho Mtakatifu, Masihi, ambalo linamaanisha Aliyetiwa Mafuta, itambidi kumfunulia huyo mwanamke hicho ni nini.

<sup>234</sup> Ni wangapi wanaojua ya kwamba Yeye alitambua mawazo yao na alijua yote kuwahu? Hiyo ni kweli. Sasa, hiyo ilikuwa ndiyo ishara ya Masihi. Nyote mtaamini? Acha awe ndiye hakimu.

<sup>235</sup> Sasa, kama ningekuja na kusema, “Mama, wewe ni mgonjwa, niweke mikono yangu juu yako, haleluya, utapata afya,” hiyo ni njia nzuri ya Kipentekoste, na hiyo ni kweli pia, ni kweli kabisa, bali angekuwa na haki ya kutilia shaka, maana asingejua kama niliagizwa kufanya hivyo au la.

<sup>236</sup> Lakini sasa, vipi kama Roho Mtakatifu akirudi nyuma na kumwambia jambo fulani baya, jambo ambalo amefanya, jambo ambalo atajua kama ni kweli ama si kweli? Basi hilo. . . Kama anajua kilichokuwako, hiyo inathibitisha ya kwamba Yeye anajua kitakachokuwako. Hiyo ni kweli, ndugu? Mnaamini hilo? Ni changamoto ya jinsi gani! Nimeona hili likitukia mbele ya watu nusu milioni kwa wakati mmoja.

<sup>237</sup> Sasa, nimekuwa nikihubiri kwa bidii, ni upako tofauti, kwa hiyo ingenibidi kuzungumza na huyu mwanamke kwa muda kidogo tu kuona kile. . . upako ungekuja. Lakini Mungu na ashukuriwe, huu hapa. Kama mtu yeyote alipata kuona picha hiyo ya Malaika wa Bwana, hebu tuone mikono yenu ikiinuliwa juu. Hakika. Ina hatimiliki ulimwenguni kote.

<sup>238</sup> Nuru iyo hiyo, Nguzo ya Moto, mnayoiona kwenye picha hiyo, ambayo sayansi imechunguza (George J. Lacy, mkuu wa FBI, aliichunguza, akasema, “Nuru iliigusa lenzi Bw. Branham. Jicho hilo la kimitambo la kamera halitapiga picha saikolojia.”), Nuru hiyo imening’inia kati yangu na mwanamke huyu. Kwenye Siku ya Hukumu, mtaona ya kwamba hiyo ni kweli. Hivi hamwezi kuiona *Hiyo?*

<sup>239</sup> Mwanamke huyo anarudi nyuma kutoka kwangu. Huyu Mama anaagua ugonjwa mbaya sana wa wasiwasi, naye ana matatizo ya kiroho yanayomsumbua. Hiyo ni kweli, sivyo? Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako.

<sup>240</sup> Sasa, unaamini? Sasa, kwa kuwa huenda mtu fulani amesema, “Ulibahatisha hilo, Ndugu Branham,” hebu nizungumze naye zaidi kidogo. Yeye ni mtu mzuri na ule upako uko juu yake. Hebu niwaambiemi tu jambo hili: Simjui huyu mwanamke, kamwe sijazungumza naye mpaka sasa hivi. Lakini mwanamke huyo anajua ya kwamba kitu fulani kiko juu yake sasa hivi, hisia tamu kweli, takatifu. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako, mama.

Sasa, yeye ni Mkanada hapa pamoja nanyi. Mnaona, ninaiangalia moja kwa moja. Hiyo . . . Si mng’ao, ni mweko, Nuru ya zumaridi, moja kwa moja kumzunguka huyu mwa- . . .

<sup>241</sup> Unasema, “Unaionaje na mimi siioni?” Vema, ni kiwango kingine.

<sup>242</sup> Paulo alionaje ile Nguzo ya Moto kule chini, na wale waliokuwa pamoja naye huko hawakuiona? Mnaona? Yule mamajusi alionaje ile nyota iliyowaongoza kwa Yesu, wala hakuna kituo cha uchunguzi kilichowahi kuiripoti? Nyota ya ajabu angani kwa muda wa miaka miwili, hakuna mtu aliyeiona ila wale mamajusi, maana wao tu ndio waliokuwa wakiitazamia.

<sup>243</sup> Sasa, sijui nilichokwambia, njia pekee ni juayo ni kwenye kanda hiyo *huko* chini, lakini lolote lililosema lilikuwa ni kweli. Sasa, hebu tu tuone tena: Naam, wasiwasi, shida yako inakuja hasa yapata wakati huu wa mchana, jioni sana wakati umechoka sana, umedhoofika, unapata hisia za kigeni sana, hisia za uchovu zinakuja. Hiyo ni kweli. Unashikwa na wasiwasi mara moja moja na kuangusha vitu.

<sup>244</sup> Si muda mrefu uliopita, ulikuwa umesimama karibu na dirisha wakati jua lilipokuwa likitua, ukashikwa na wasiwasi sana, ukausugua mkono wako. Hiyo ni kweli. Ningejuaje mahali ilipokuwa umesimama? Ningejuaje kwamba ulifanya hivyo? Kabla hujaja mkutanoni, ulimwomba Mungu kwamba ungepata kadi ya maombi. Ulifurahi sana ulipoipokea, hiyo ni BWANA ASEMA HIVI. Hiyo ni kweli.

<sup>245</sup> Hili hapa jambo lingine: Mungu ananiambia ya kwamba moyoni mwako, unamwombea mtu mwingine, huyo ni rafiki anayekufa, aliye na kansa. Hawaishi hapa, wanaishi Fort Saint John, naye huyo mtu ametiwa uvuli kwa kivuli cheusi, mtu huyo ni mwenye dhambi, akifa kwa kansa, BWANA ASEMA HIVI.

<sup>246</sup> Je, mambo hayo ni ya kweli? Inua mkono wako. Sasa kuna kivuli cha shaka niani mwako? Yeye ni Yesu Kristo? Je, Mungu yuko miongoni mwa watu Wake? Unaamini, Dada? Chukua lesa iyo hiyo uliyo nayo, iweke juu ya mtu huyo wala usitie shaka, Yesu Kristo atamponya. Nenda, amini.

<sup>247</sup> Unaamini kwa moyo wako wote? Mtu yeyote anawezaje kumwambia mtu wao ni akina nani, na mahali wanakotoka, kile walichofanya kabla hawajaja hapa, na yale waliyofanya majuma

mawili au matatu yaliyopita, na wanachowazia niani mwao, na kwamba wanamwomba nani, ila Mwenyezi Mungu?

Sasa, hiyo ni kweli, ndugu? Ninawatakeni mjue ya kwamba Kristo yu hai.

248 Unaamini, Bw. Durney? Unaamini kwa moyo wako wote? Basi likubali. Nenda, ukaketi chini na uamini kwa moyo wako wote na shida yako imekwisha. Mungu akubariki. Ninataka ninii yake. . . Amina.

249 Niliona kivuli hicho kikija juu ya huyo mtu. Mwamini Bwana, Bw. Durney, mkubali kama Mwokozi wako binafsi, usiwe na shaka, nami nitakutana nawe kule kwenye ile Njia kuu ya Wanyamapori.

250 Hatufahamiani, mama. Sikujui, lakini Mungu anakujua, hiyo ni kweli, sivyo? Unaamini kama Mungu anaweza kunifunulia shida yako kwamba utaamini kwamba ni jambo la kibinafsi kwako? Kusudi watu wajue ya kwamba hatufahamiani, hebu na tuinue tu mikonu yetu namna *hii*.

251 Sina habari, unaonekana kama mwanamke mzuri, mwenye afya kwangu mimi. Lakini unaugua kivimbe, na kivimbe hicho kinasababisha viungo vingine kutofanya kazi, hivyo ni figo yako na kibofu chako. Hiyo ni kweli. Unaamini? Vema. Yesu Kristo atakufanya mzima. Nenda, amini kwa moyo wako wote.

Unaamini sasa? Iweni tu na imani. Msiwe na shaka.

252 Unaniamini mimi kuwa ni mtumishi Wake? Huko hapa kwa ajili yako mwenyewe, uko hapa kwa ajili ya mume wako. Yeye ni mtu ambaye hajaokoka nawe unamwomba. Hiyo ni kweli. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Nenda, amini.

253 Mnajua yale yule akida wa Kirumi aliyosema, kama nilivyosema, "Mwamini Bwana Yesu Kristo, nawe pamoja na nyumba yako mtaokoka." Vipi. . .? Je, hiyo ilimaanisha kwa sababu aliamini, nyumba yake ingeokoka? La. Kama ana imani ya kutosha kwa nafsi yake, anaweza kuwa na imani ya kutosha kwa ajili ya nyumba yake. Amini kwa moyo wako wote nawe pamoja na mpenzi wako mtaishi pamoja katika Paradiso hiyo ya Mungu ng'ambo ya mto. Mungu akubariki. Nenda ukapokee ulichoomba.

254 Sasa mnaona, kila kitu kimeanza, kunipofusha. Mnaona? Ninakuwa, ni vigumu kwangu kuliona kusanyiko kwenye wakati huu. Iweni na kicho sasa, kicho kabisa.

255 Sikujui, mama. Sasa, mahubiri hayo yote, kwa yapata saa mbili, na hata hivyo hayakunitatiza hata kidogo, lakini angalieni tu, yapata maono matatu ama manne tu na yale yamenifanyia sasa, ninakuwa dhaifu sana. Mnaona?

256 Ni wangapi wanaojua ya kwamba Yesu, mwanamke aligusa vazi Lake Naye akatambua ya kwamba nguvu zilikuwa zimetoka? Hiyo ni kweli? Hizo ni nguvu zimetoka.

257 Mama aliyeketi papa hapa nyuma, akiteseka. Utaamini kwa moyo wako wote! Una ugonjwa wa moyo, shida ya macho yako, wasiwasi. Unaamini kwa moyo wako wote? Yule mama kutoka Grande Prairie, Binti Thompson, amini kwa moyo wako wote na uponywe, katika Jina la Yesu Kristo. Utaamini? Vema.

258 Sikujui, hatufahamiani. Kama Yesu atanifunulia shida yako, utaniamini mimi kuwa ni nabii Wake, ama, samahani, mtumishi Wake? Neno hi—hilo, *nabii*, kwa namna fulani linawakwaza watu, hiyo ndiyo sababu nilisema. . . Jambo fulani tu nililotaka kumwambia huyo mwanamke, sababu ya mimi kuifunika maikrofoni kwa mkono wangu.

259 Sisi ni watu wawili waliokutana, labda kama Bwana wetu na yule mwanamke kisimani, labda alikuwa ni msichana. Lakini unaugua ugonjwa wa koo lako. Hiyo ni kweli. Ulisababishwa na polio. Hiyo ni kweli. Kama Mungu ataniambia wewe ni nani, utaniamini mimi kuwa ni mtumishi Wake? Bibi Duncan, wewe nenda nyumbani na uwe mzima katika Jina la Yesu Kristo.

Usiwe na shaka.

260 Unayeketi upande huu papo hapo, ukimwombea mke wako ambaye hajaokoka, bwana. Unaamini Mungu atamwokoa na. . .? Vema, unaweza kupata ulichoomba, Mungu hujibu maombi yako.

261 Ni nani huyo mama ambaye ndiyo kwanza apite, akishuka kwenye marefu ya kanisa? Uliombewa? Uliombewa sasa hivi? Loo. Niliiona ile Nuru pe—pembeni. Loo, naona ni yule mtu mwenye ugonjwa wa mgongo anayeketi pale. Bw. Pettigrew, amini kwa moyo wako wote, Yesu Kristo atakuponya. Mpendwa wako ana yabisi kavu, amini kwa moyo wako wote nao watapata afya.

262 Kama unaweza kuamini kwa moyo wako wote, mambo yote yanawezekana. Ni wangapi wenu mnaoamini sasa kwa moyo wenu wote? Ninakuwa dhaifu sana, linaniyumbisha tu kila mahali, pande zote. Ni wangapi walio na. . .?

Wamekwisha huko, mtu mwingine aliye na kadi za maombi upande huo, aingie mstarini, upande huo.

Ni wahudumu wangapi hapa wanaoamini ya kwamba huduma hii ni Bwana Yesu Kristo, inueni mikono yenu. Wahudumu.

263 Ninataka, nisiliache kusanyiko hili katika hali kama hii, kuwafanya nyote mfikirie ya kwamba mimi ndimi pekee niliye na haki ya kuwaombea wagonjwa, mchungaji wenu ana haki ya kuwaombea ninyi kama tu niliyo mimi. Sasa, huenda asiwe mwonaji, wanakuja mmoja tu katika kizazi. Lakini mimi—mimi. . .

264 Mnakumbuka, Mungu kamwe hakuwahi wakati mmoja. . . Kwa hiyo hilo litaondoa jambo fulani linalosumbua akili zenu

ambalo tayari ninaweza kulitambua. Katika Biblia hapakuwapo ila wakati mmoja tu. . .mwonaji mmoja kwa wakati mmoja, Eliya, halafu Elisha, na halafu Isaya, na kisha Yeremia. Mnaona? Hiyo ni kweli. Mnaona? Lakini. . . Ni. . .

Watu wote walio na kadi ya maombi C simameni upande huu, upande huu, tafadhalini, kadi za maombi C.

<sup>265</sup> Ninataka kujua wahudumu hapa ambao wangekuja hapa na kusimama hapa chini pamoja nami na kusaidia kuwaombea wagonjwa kwa dakika moja tu. Naweza kuwachukua baadhi yenu ndugu? Ili kusanyiko lenu hapa lione ya kwamba ninyi ni wana wa Mungu. Nina furaha sana kujua ya kwamba ninyi ni wana wa Mungu.

Jamani, unapaswa kuwa mwaminio kwenye wakati huu muhimu sana. Usijali kuhusu huyu mtoto, atakuwa mzima.

<sup>266</sup> Sasa, sijui kama tungeweza. . . Shukeni moja kwa moja hapa chini, ndugu. Hebu tuondoke, tuondoke jukwaani. Simameni tu, fanyeni mistari miwili hapo, moja kwa moja juu na chini namna hiyo. Naam, ndugu, naam.

<sup>267</sup> Njoo papa hapa, Dada. Tembea papa hapa mstarini, hebu kidogo tu. Aisee, jambo lingine, tayari umeponywa, kwa hiyo haikubidi kupitia mstarini, unaweza tu kwenda nyumbani.

<sup>268</sup> Sasa, njoni upande huu, kusudi waweze kurudi kwenye mstari huu. Sasa, ninawatakeni baadhi yenu ndugu mje papa hapa, msimame papa hapa chini. Ninawatakeni msimame papa hapa, nataka, msimame pamoja nami. Ninawatakeni ninyi ndugu, sasa, msimame hapo, kwa muda kidogo tu, ngojeni, shukeni mpate kuwawekea wagonjwa mikono. Vipi kuhusu, Ndugu, wewe simama karibu na ndugu huyu papa hapa, mmoja wenu. Hilo ni zuri.

Sasa, njoni papa hapa, fanyeni mstari ili kila mmoja wenu aweze kuombewa. . .

Sasa, enyi kusanyiko, nawatakeni mfahamu, Biblia ilisema, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio."

<sup>269</sup> Kuna maskini mama mmoja hapa ambaye nilikuwa na mahojiano naye asubuhi ya leo, naye alikuwa huko Grande Prairie. Mimi. . . Yeye ni mteja wa kanda wa Ndugu Leo Mercier, Ndugu Gene Goad, nao waliniambia nintafute, Dada Brown.

<sup>270</sup> Na kwa hiyo ye—yeye alikuwa kwenye mkutano wa Grande Prairie. Ndipo Roho Mtakatifu akamwambia kuhusu mwanamke aliyekuwa na (nafikiri, jina lake lilikuwa nani? Huyu ni Brown, ama, Binti Dada Brown), alikuwa na wa—waridi kwenye kofia yake, na kumwambia kuhusu hali zake, na bila shaka, sikuwa nimewahi kumwona maishani mwangu. Ndipo nikasema, "Kila mmoja wekeaneni mikono mmoja juu ya mwingine." Huenda mama huyo yuko hapa alasiri ya leo. Nikasema, "Kila mmoja wenu wekeaneni mikono."

271 Ndipo kila mtu wakawekeana mikono, kwa sababu Biblia ilisema, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio, wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa watapata afya.” Ndipo basi mimi. . . Walipofanya hivyo. . .

272 Sababu ya mimi kufanya hivyo, ndugu, ni kwa ajili yenu kusanyiko. Msingoje mpaka Oral Roberts, ama mtu fulani aje, ama mhudumu fulani aliye na huduma ya hiyo, ndugu zenu, wachungaji wenu kweli. . . Mniamini mimi kuwa ni mtumishi wa Mungu? Ninawaambia katika Jina la Bwana, watu hawa wana mamlaka yale yale kuwaombea kama mtu yeyote alivyoyao, wao ni watumishi wa Mungu. Mhudumu yeyote anayeamini katika uponyaji wa Kiungu, awe ni Mmethodisti, Mbaptisti, Mlutheri, Mkusanyiko ama chochote kile, kama anamwamini Mungu, ana haki ya kuwaombea wagonjwa.

273 Na sasa, angalieni, maskini mama huyo, aliweka mikono yake juu ya mtu fulani, na mara akahisi mkono mmoja umewekwa juu ya wake, ambao ulikuwa mkubwa zaidi. Ndipo akaangalia kote, hapakuwapo na mtu karibu naye. Kina mama waliokuwa nyuma yake, alijua, nao hawakumwekea mikono yao, basi akauhisi mkono huo, naye akasema alitetemeka tu kwa nguvu za Mungu.

274 Halafu asubuhi ya leo, kwenye meza ya kiamshakinywa, nilikuwa nikila chakula cha kutwa pamoja naye huko, ama, kiamshakinywa kwenye Hoteli ya Windsor, ndipo Roho Mtakatifu akasema, “Anataka umwekee mikono.” Nami nikasema, “Nifanye nini, Baba? Ishara Yako itakuwa ni nini?” Alikuwa upande wa pili wa meza, katikati yetu kulikuwa kumewekwa sahani za kila namna. Kasema, “Atauchukua mkono wake na kuzirudisha nyuma sahani hizo, akifanya njia nyofu upate kuweka mkono wako upande wa pili juu ya wake.

Na papo hapo, akanyosha mkono na kurudisha vyombo nyuma, bila kujua. Nikasema, “Dada, kwa nini ukafanya hivyo?”

Akasema, “Kitu fulani ndio kwanza kiniambie nifanye hivyo.” Hilo lilitosha kwake.

275 Dada, uko humu jengoni sasa? Uko hapa alasiri ya leo? Dada Brown? Dada Brown? Amesimama papa *hapa*. Yuyu huyu. Mnaona? Yeye ni Mungu, sivyo?

276 Sasa, ninataka kila mtu hapa ndani, aangalie akisimama kwenye mstari huu, na mara mstari huo utakapokwisha, acha kadi hizo zingine za maombi ziendelee kuja huku. Halafu. . . [Mtu fulani anazungumza na Ndugu Branham—Mh.] (Huh?) Kadi zote za maombi ziendelee tu kupanga mstari hapa. Halafu basi, baada ya wao kumalizika, wote wasio na kadi za maombi na wanataka kuombewa, mnaweza kujipanga moja kwa moja nyuma yao.

Sasa, kabla hatujafanya hivyo, hebu sote na tuinamishe vichwa vyetu kwa Mwenyezi Mungu.



277 Vipi kama huyu alikuwa ni mama yako aliyesimama mstarini? Vipi kama huyu alikuwa mke wako? Vipi kama ilikuwa ni dada yako? Vipi kama ilikuwa ni mama yako, ama binti yako, ama mwanao? Kumbukeni, ni wa mtu fulani. Je, ungetaka kila mtu awe mwaminifu kama huyo alikuwa ni mama yako, ama mke wako, mama wa mtoto wako mchanga, anayekufa, amejaa kansa? Hivi hungetaka mtu fulani aombe kwa uaminifu? Sasa, ninyi ombeni.

278 Baba wa Mbinguni, ninamwasilisha, alasiri ya leo, kwanza kabisa kwa kipawa cha Kiungu, Yesu aliyefufuka, kuthibitisha ya kwamba Yeye yuko miongoni mwa watu Wake, apate kujionyesha Mwenyewe yu hai. Na sasa, baadaye, pili, ninawawasilisha watumishi Wako, hawa wahudumu, watu uliowaita. Baadhi yao wamekuwa wakihubiri miaka mingi, mingi sana kuliko mimi, wao wana sifa bora zaidi, kama wahudumu, kuliko mimi mwenyewe.

279 Nami nataka kusanyiko lijue ya kwamba mchungaji wao ni mtumishi Wako, kwa hiyo mimi, kwa karama ya Kiungu, nimekuwasilisha Wewe kwao, sasa ninawawasilisha watumishi Wako kwao. Nami ni mmoja pamoja nao, Baba, mtumishi Wako. Nasi tunalichukua Neno la Bwana wetu.

280 Sasa, Bwana Yesu, Wewe unajua kweli yote, wala kamwe hutauheshimu uongo. Na imethibitishwa mara makumi elfu kote ulimwenguni, bila kushindwa hata kumoja kwa hayo maono, ambayo yanathibitisha kwamba ni kweli. Mbele ya utafiti wa kisayansi, mbele ya vibaini uongo, mbele ya kamera na kahalika, Wewe umethibitisha kuwa ni Mungu.

281 Na sasa, Wewe ni Mungu alasiri ya leo. Nawe ulitoa tamshi hili, jambo la mwisho ulilosema ulipokuwa ukiondoka: “Enendeni ulimwenguni kote, mkaihubiri Injili. Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio,” na hawa ni waaminio, Bwana, Wewe ulisema, “katika Jina Langu watatoa pepo; watasema kwa lugha mpya; wakishika nyo—nyoka, au kunywa kitu cha kufisha, hakipaswi kuwadhuru; na wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya.”

282 Sasa, Baba, ulijithibitisha Mwenyewe kuwa hai kulitimiza Neno Lako, unalilinda Neno Lako kulithibitisha. Na sasa ninamwasilisha kwa jamii hii, na kwa maeneo kote hapa, Yesu Kristo na watumishi Wake. Nasi, kama watumishi Wako, Bwana, tutafuata maagizo Yako, bila kujali ulimwengu usioamini unasema nini juu yake. Tutaweka mikono yetu juu ya watoto Wako wagonjwa, wanaoteseka, nasi tunaamini ya kwamba watapata afya. Tunakukubali Wewe kama Mponyaji wetu sasa hivi.

283 Kila mtu katika mistari ya maombi, wale wanaokuja kwenye mistari ya maombi, ninawaomba sasa, katika Jina la Yesu Kristo, kumkubali Yesu kama Mponyaji wenu. Msitie shaka. Wakati

watu hawa wa Mungu, nasi tunaweka mikono yetu juu yako, wewe. . .kuna kitu kimoja tu kingekuzuia usipone, hicho ni kutokuamini kwako. Usikose kuamini, bali mwamini Mungu.

<sup>284</sup> Nasi tumesimama hapa sasa, tukiwaombea mnapopita karibu na kusanyiko hili, isitoshe, bali watu mia tatu ama mia nne waliokusanyika hapa alasiri ya leo watakuwa wakiwaombea. Na kila ombi. . .Na sasa aminini.

Sasa, kwa ajili ya maombi ya kukemea, huku vichwa vyenu vimeinamishwa:

<sup>285</sup> Shetani, sisi, kama Kanisa la Mungu, tunaongea nawe moja kwa moja. Wewe ni ibilisi, mtesi, nawe umewafunga watumishi wa Mungu kwa roho yako ya udanganyifu. Kwa hiyo sisi kama wanadamu hatuna nguvu dhidi yako, kwa hiyo hatuji kukutana nawe katika jina la kanisa, ama dhehebu fulani, bali, yameshindwa, bali tunakuja kukutana nawe katika—katika Jina la Mshindi wetu, Yesu Kristo. Tunalitukuza Jina Lake na Uwepo Wake mbele za watu, kama Mshindi wa kila maradhi na kila ugonjwa, kwamba yamewekwa chini ya miguu Yake. Na sisi kama watumishi Wake tunatekeleza agizo Lake.

<sup>286</sup> Tunakuapisha katika Jina la Yesu Kristo: Mwachilie kila mmoja wa watu hawa! Tutafuata agizo Lake kwa kuweka mikono juu ya wagonjwa, nao watapata afya, kwa kuwa tunalinena, katika Jina la Yesu Kristo.

Amini tu, amini tu. . .

<sup>287</sup> Vema, kila mtu aombe sasa, wakati wagonjwa wanapopita.



61-0521 Utuonyeshe Baba  
United Church  
Dawson Creek, British Columbia Canada

SWAHILI

©2024 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS  
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.  
[www.branham.org](http://www.branham.org)

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

[www.branham.org](http://www.branham.org)